SUPA MULTIBET BONUS
SportPesa
SHINDA HADI 750x YA USHINDI WAKO.
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mapigano** kugombea malisho ya mifugo yasababisha vifo

UKURASA 2



LUKAKU: SIONDOKI CHELSEA

UKURASA 21


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 15, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580946

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# KICHEKO

• **Mishahara** yapandishwa, kikokotoo kipya cha mafao mikononi mwa Rais... *Endelea ukurasa 2*




Wachuuzi wakiendelea na biashara zao, kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Mwisho, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya kuwapo kwa kibao cha amri ya kuzuia kufanya biashara katika eneo hilo kilichowekwa na Manispaa ya Ubungo. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wakuu wa mikoa na wilaya waonywa kutomtendea haki Rais

UKURASA 2



## Ripoti ya uchunguzi chumvi ya wanyama yaanika 'madudu'

UKURASA 4

MICHEZO YANGA, DODOMA HAPATOSHI LEO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa, Shaka Hamdu Shaka (katikati), akipewa rungu na Laiguanani Mkuu wa jamii ya watu wa Simanjiro, ikiwa ni ishara ya kumsimika kuwa kiongozi wa ngazi ya juu katika jamii hiyo na kumpa jina la "Ole Shaka", alipowasili mkoani Manyara jana, kwa ziara ya siku mbili kukagua uhai wa chama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kicheko mishahara kupanda kwa 23.3%

**Na Mwandishi Maalum**

NI kicheko! Ndivyo ambavyo unaweza kusema kutokana na Rais Samia Suluhu Hassan kuridhia mapendekezo ya nyongeza ya mishahara, ikiwamo kima cha chini kwa watumishi wa umma kwa asilimia 23.3, Ikulu imetangaza.

Hatua hiyo itakayotekelezwa kuanzia mwaka ujao wa fedha, yaani kuanzia Julai mwaka huu, inahitimisha kilio cha takriban miaka saba cha watumishi wa umma kutoshuhudia nyongeza ya mishahara yao.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhuru Yunus, mapendekezo hayo yaliyowasilishwa Ikulu, ni mwendelezo wa kikao cha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alichokifanya hivi karibuni mkoani Dodoma na kupokea taarifa ya wataalamu kuhusu nyongeza ya mishahara.

"Nyongeza hiyo imefanyika kwa kuzingatia Pato la Taifa (GDP), mapato ya ndani yanayotarajiwa kukusanywa katika mwaka 2022/23 na hali ya uchumi wa ndani na nje," Zuhura alifafanua katika taarifa yake hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Ikulu, kutokana na hatua hiyo, katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imepanga kutumia Sh. trilioni 9.7 kwa ajili ya kugharamia malipo ya mishahara ya watumishi wote wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Wakala za Serikali.

"Hivyo, bajeti ya mishahara ya mwaka 2022/23 ina ongezeko la Sh. trilioni 1.59, sawa na asilimia 19.51 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22," Zuhura alifafanua katika taarifa yake hiyo.

**KIKOKOTOO KIPYA**

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo alibainisha kwamba Rais Samia amepokea mapendekezo ya kanuni mpya ya mafao ya pensheni kama Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) lilivyoomba Mei Mosi mwaka huu.

Zuhura alibainisha kwenye taarifa yake hiyo kuwa Rais ameridhia na kuielekeza wizara yenye dhamana na masuala ya hifadhi ya jamii kuendelea kushirikiana na TUCTA na Chama cha Waajiri nchini (ATE) ili kukamilisha taratibu za kuhakikisha malipo ya mkupuo ya asilimia 25 yaliyokataliwa na wadau mwaka 2018 yanapandishwa hadi asilimia 33.

# CCM yawaonya ma-RC, ma-DC

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema kuna ukimya kwa wakuu wa mikoa na wilaya katika kuelezea mafanikio ya serikali.

Shaka alisema hayo jana mjini Babati mkoani Manyara katika mkutano wa ndani wa kujitambulisha mbele ya wanachama wa CCM kama mlezi mpya wa chama hicho akichukua nafasi ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda.

"Wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya kote nchini mna jukumu la kuyaeleza mafanikio ya serikali ya Mama Samia, sasa hivi kuko kimya hammtendei haki Rais wetu," alionya.

Shaka alisema kuwa katika utafiti alioufanya, miaka miwili iliyopita kila mkuu wa mkoa na wilaya alikuwa akitoa taarifa za mafanikio ya serikali, jambo ambalo ni tofauti na hali ilivyo sasa.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wake, Rais Samia amefanya makubwa kana kwamba amekaa miaka mitano, ikiwamo kuifungua Tanzania kiuchumi na kidiplomasia.

"Rais Samia ni kinara wa demokrasia katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, hili liko wazi. Lazima tuyaseme mafanikio hayo," alisema Shaka aliyekuwa anazungumza kwa ukali.

Alisema kuwa Rais Samia toka aingie madarakani, amechukua hatua kadhaa za kulainisha uhasama na kuponya vidonda.

# Mapigano kugombea malisho ya mifugo yasababisha vifo

**Na Richard Makore**

WATU watatu wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa wilayani Igunga mkoani Tabora katika mapigano ya kugombea maeneo ya kulishia mifugo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Richard Abwao, alisema tukio hilo lilitokea juzi katika eneo la Isakamaliwa wilayani Igunga.

Alisema wananchi hao ambao walikuwa wanagombea maeneo ya kulishia mifugo, walitumia silaha za jadi kutekeleza mauaji hayo.

Kamanda Abwao alisema chanzo cha ugomvi huo ni kugombea sehemu ya kulishia mifugo yao na kwamba tayari msako wa kuwapata watuhumiwa wengine unaendelea baada ya watu wanne kukamatwa hadi jana kwa tuhuma za mauaji hayo.

Aliongeza kuwa matukio kama hayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu na kwamba ameagiza askari wake kuimarisha ulinzi wa usiku na mchana katika eneo hilo.

Kamanda Abwao alisema mtu mmoja aliyejeruhiwa katika tukio hilo anaendelea kupata matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga.

"Tumeweka ulinzi mkali katika eneo yalipotokea mauaji hayo na polisi watakuwapo saa 24 usiku na mchana ili kuhakikisha watu hawalipizi kisasi," alisema.

Kamanda huyo alisema mkakati wa kumaliza mgogoro huo uligharimu maisha ya watu umeanza kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya hiyo.

"Lazima tuweke mipango endelevu ili kuhakikisha mauaji kama hayo hayatokei tena ili jamii iweze kuishi kwa amani muda wote," alisema.

# Matukio 1,300 ya ukatili yaripotiwa miezi mitatu

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amesema ndani ya kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu kumeripotiwa matukio 1,361 ya ukatili wa kijinsia katika mkoa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani inayoadhimishwa leo, Mrindoko alisema jana kuwa ndani ya matukio hayo, kuna matukio 887 yanayohusu ukatili dhidi ya watoto. Mrindoko alisema visa vinavyoongoza katika takwimu hizo ni ubakaji, ulawiti, kutelekeza familia, ajira za watoto, vipigo na mimba za utotoni.

"Niombe sana familia kutenga muda wa kukaa pamoja kujadili mambo ya kifamilia, kufanya uamuzi na mipango ya pamoja. Hii inajenga upendo na mshikamano ikiwa ni pamoja na kufahamu maendeleo ya watoto nyumbani hadi shuleni na kuwapeleka sehemu za ibada ili kujenga jamii imara," alisema. Mrindoko alizitaka familia zote kutimiza wajibu wao katika malezi ili kuondokana na wimbi la familia zinazotelekezwa pamoja na watoto wa mitaani.

"Familia ikipata mahitaji muhimu ya chakula, malazi, mavazi, ulinzi na upendo, ninaamini kabisa mambo haya ya ukatili hayawezi kutokea," alisema. Mkuu wa Mkoa alisema vitendo vingi vya ukatili dhidi ya watoto vinafanywa na wanafamilia wenyewe, hivyo akaitaka jamii kuhakikisha inachukua hatua kuhakikisha mambo hayo yanakomeshwa.



Watoto katika Jiji la Mbeya, wakiwa wametoka kukusanya kuni katika Barabara ya Mbalizi, jijini humo mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia nyumbani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# India yatoa fursa kwa wabunifu wa Tanzania

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa India nchini kupitia kituo chake cha utamaduni wa India cha Swami Vivekananda, umewakutanisha wabunifu wa sanaa za ufundi na uchoraji wa Tanzania kuonyesha kazi zao ili kumwenzi mama na kuzitangaza kimataifa.

Wabunifu hao wamepata fursa ya kuonyesha kazi mbalimbali wanazofanya kupitia maonyesho ya sanaa za ufundi na uchoraji yaliyoandaliwa na Kituo cha Swami Vivekananda kilichopo jijini Dar es Salaam.

Akifungua maonyesho hayo juzi, Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alisema jumla ya wabunifu 36 wa Kitanzania wameshiriki kuonyesha kazi mbalimbali walizozifanya kupitia sanaa za ubunifu na uchoraji.

Alisema miongoni mwa walioshiriki maonyesho hayo ni wanafunzi ambao nao wamepeleka kazi zao walizozifanya baada ya kituo kutoa fursa ya watu kuomba kushiriki.

"Maonyesho haya yameandaliwa ikiwa ni katika kuadhimisha Siku ya Mama Duniani, katika jamii zetu mama ndiye anayebeba ujauzito, analea watoto, mama ana majukumu mengi.

"Leo (juzi) tumewakutanisha wabunifu 36, wengi wao wakiwa ni wabunifu vijana wa Kitanzania, baadhi ni wanafunzi na wapo wanaotoka mikoa mbalimbali ikiwamo Arusha na Mwanza," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la maonyesho hayo ni kutangaza kazi za ubunifu zinazofanywa na wabunifu wazawa na hiyo inatokana na ushirikiano mwema na wa muda mrefu baina ya Tanzania na India.

Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangamale, aliushukuru Ubalozi wa India pamoja na kituo chao kwa kutambua kazi za ubunifu zinazofanywa na Watanzania.

Alisema tathmini iliyofanywa na Baraza la Sanaa la Taifa inaonyesha Tanzania kuna wasanii milioni sita na zaidi ya milioni nne wanajihusisha na sanaa za ufundi.

"Shida kubwa tuliyonayo ni soko, soko limekuwa dogo na hayana ubora, kwa hiyo fursa kama hizi zinasaidia wasanii kutangaza kazi zao na kuziuza.

"Wasanii wanaacha hizi kazi kwa sababu wanaona haziwalipi, tunaomba Watanzania watuunge mkono kuja kwenye maonyesho haya," alisema.

Msanii Mkazi kutoka Idara ya Sanaa Bunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Safina Kimbokota, alisema amewasilisha kazi tatu katika maonyesho hayo zikiwa zimebeba ujumbe tofauti wa kumwelezea mama.

"Mama ni nguzo katika familia, anatakiwa kuheshimiwa, kupendwa, kupewa ushirikiano. Kazi yangu ya kwanza inakumbusha wajibu kwa jamii kumwangalia mama katika hali ya kipekee.

"Kazi ya pili inaitwa gift (zawadi) inaonyesha mkono umebeba mtoto, hii inazungumzia kuwa tupo duniani kwa sababu ya mama, kazi ya tatu inaitwa 'focus' inaonyesha uso wa mama ukimwangalia mtoto, hii inamaanisha pamoja na matatizo ya wanawake wanapitia lakini mwisho wa siku anabarikiwa na mtoto," alifafanua.

Kuhusu maonyesho hayo, msanii huyo alisema Siku ya Mama Duniani ni muhimu ndiyo maana wamekutana kusherehekea, kutambua na kuhamasisha umuhimu wa mama duniani.

Alisema maonyesho hayo yanamsaidia kujifunza fikra na mawazo ya wabunifu kutoka kwa wenzake kupitia kazi zao walizowasilisha na kujitangaza katika soko la kimataifa.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni wa India, Santhosh Raja, aliishukuru Idara ya Sanaa Bunifu ya UDSM kwa kutumia muda wao kushirikiana na kituo hicho kuandaa maonyesho hayo.

# Ridhiwani ataka watumishi ardhi watende haki

**Na Waandishi Wetu,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewataka watumishi wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha wanatoa haki wakati wa kutekeleza majukumu yao kwa wananchi.

Amesema utoaji haki uko katika sura tofauti kuanzia utoaji hati, upatikanaji haki katika mabaraza ya ardhi na nyumba sambamba na utoaji taarifa na uwezeshaji wananchi katika ardhi au rasilimali ardhi.

Amesema baadhi ya watendaji wa sekta ya ardhi wamekuwa miungu watu kwenye maeneo yao kuliko hata Rais wa nchini ambaye ardhi yote iko chini ya mamlaka yake na kubainisha kuwa mwananchi anaweza kwenda ofisi ya ardhi kwa ajili ya kumilikishwa ardhi lakini adha anayoipata wakati wa kuomba kupata uhalali wa kumiliki ardhi yake, ni kubwa kutokana na maofisa 'kujizungusha' bila kumsaidia.

"Kama nilivyokwishasema, yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, ubabaishaji ufike mwisho, tumeelewana ndugu zangu?" Ridhiwani alihoji alipokutana na watumishi wa sekta ya ardhi Mkoa wa Mbeya, alikoonyesha kutoridhishwa na utendaji kazi wa baadhi ya watumishi wasio waadilifu.

"Kama kuna mtumishi anadhani kuna suala la kula kula ovyo kwenye wizara hii, basi siyo kwa nyakati hizi. Ndugu zangu watendaji wenzangu ninaomba tuwe waadilifu katika kutenda haki kwa wananchi," alisema.

Naibu Waziri huyo pia aliwataka maofisa mipango miji wa Mkoa wa Mbeya kuwa na mipango bora ya mipango miji ili Jiji la Mbeya lisiendelee kuwa jiji la makazi holela.

Kwa mujibu wa Ridhiwani, ukiwa kwenye ndege unaona milima ya Mbeya imejengwa majengo kwenye ardhi isiyopimwa, akiwataka maofisa mipango miji hao kutosubiri watu kuendeleza makazi holela na baadaye kujitokeza kurasimisha maeneo hayo.

Ridhiwani yuko mkoani Mbeya kwa ziara ya siku mbili. Mbali na kufanya kikao na watumishi wa sekta ya ardhi, ameshiriki utoaji hati na leseni za makazi kwa wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja na wale wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA.

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 15.05.2022 hadi 29.05.2022 kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 21, Upana - Mita 4.3, Kimo -Mita 5.3**
3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu

**( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Uchunguzi wabaini 'madudu' mengi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
NGORONGORO

KAMATI iliyoundwa kuchunguza uhalali na ubora wa chumvi maalum kwa ajili ya kulishia mifugo katika Tarafa ya Ngorongoro imekabidhi ripoti yake kwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro huku ikibaini 'madudu' mengi.

Kamati hiyo iliundwa na Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mwangwala, mwishoni mwa mwaka jana kuchunguza chumvi hiyo iliyolalamikiwa na wafugaji wa Tarafa ya Ngorongoro kuwa ni feki na haina viwango na inasababisha madhara na vifo kwa mifugo yao.

Tangu mwaka 2017, serikali kupitia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilipiga marufuku wafugaji kupeleka mifugo yao kreta ambako walikuwa wakiipeleka kupata chumvi ya asili inayopendwa na mifugo na hivyo kuiagiza Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) iwe inanunua chumvi kwa ajili ya malisho ya mifugo na kuwagawia wafugaji wa Tarafa ya Ngorongoro.



Mkuu wa wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala.

**MADUDU YALIYOBAINIKA**

Ripoti hiyo iliyokabidhiwa juzi, imebainisha kuwa mzabuni aliyepewa kazi na NCAA ya ununuzi na usambazaji wa chumvi ni kampuni ya ujenzi inayoitwa Panga Building and Construction Limited ambayo haijasajiliwa kufanya biashara ya vyakula vya mifugo kama inavyoelekezwa kwenye sheria ya Grazing Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resource) kifungu cha (5) kifungu kidogo (1) (a).

Inabainishwa katika ripoti hiyo kwamba mzabuni katika kufanya biashara hiyo, alimtumia mtaalamu wa mazingira, Mahuna B. Mahuna kinyume cha inavyoelekezwa kwenye sheria ya malisho, yaani Grazing Land and Animal Feed Resources, 2010 kifungu cha 21(3) ambacho kinamtaka mtu yeyote anayeingiza vyakula vya wanyama lazima awe na mtaalamu wa vyakula vya wanyama.

Taarifa hiyo ambayo Nipashe imeiona, pia inabainisha kwamba chumvi hiyo haiyeyuki yote kwenye maji kutokana na uwapo wa vipande vya mchanga vinavyoonekana kwa macho.

"Kiwango cha vitu vigumu kwa mujibu wa taarifa ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni kati ya 57.39 na 62.62, kiasi hiki cha vitu vigumu ni kikubwa kwa chumvi kutumika kama chakula cha mifugo," sehemu ya ripoti hiyo inabainisha.

Taarifa zote za Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na taarifa ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) zimebaini kiwango kikubwa cha chumvi cha 36.97%m/m kuliko kiasi kilichokuwa kinatakiwa kwa mujibu wa KEBS 458:2010 ambapo ni 20 30 %m/m, kipimo kinachoonekana kutumika kupima ubora wa chumvi hiyo ni kutoka nchini Kenya kwa mujibu wa nakala za barua alizotoa mzabuni.

Taarifa ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeelekeza kuwa matumizi ya chumvi nyingi yanaweza kusababisha sumu ya chumvi (Salt poisoning/ salt toxicity).

Vilevile, kiwango cha Calcium katika sampuli zote kiko juu kwa zaidi ya asilimia 3.1 ambacho kimeonyeshwa juu ya mfuko, hivyo kuashiria kwamba chumvi itakuwa imechanganywa na vitu vingine kama chokaa.

Ripoti hiyo inabainisha zaidi kuwa kiwango cha mchanga (silcon) cha wastani wa asilimia mbili katika sampuli zote kinaashiria kwamba chumvi imechanganywa na mchanga.

"Kiwango kidogo cha lead kilionekana katika sampuli iliyotoka katika Kijiji cha Misigiyo, viashiria kwamba chumvi imechanganywa na vitu vingine inapelekea kuhitimisha na kusema kwamba chumvi hii haijakidhi matakwa ya Grazing Land and Animal Feed Resources, 2010 (standards of animal feed resources) kanuni ya mwaka 2012," inabainishwa katika ripoti hiyo.

Ripoti inabainisha zaidi kuwa pamoja na kuwapo kwa viashiria vya chumvi hiyo kuwa imechanganywa na vitu vingine ambavyo havikutakiwa (adultered), timu imeshindwa kubaini kama chanzo cha tatizo hilo ni ama kiwandani, mzabuni au wakati wa mapokezi (NCAA) au ni kwa wafugaji ambako sampuli ilikusanywa.

Chimbuko la sakata hili linarejewa Desemba 20, 2021, Diwani wa Ngorongoro, Simon Saitoti, alipomjulisha Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro kuhusu malalamiko kutoka kwa wafugaji kuhusu kuwapo kwa mchanga, mawe na rangi nyekundu kwenye chumvi iliyokuwa imesambazwa kwa wafugaji ndani ya kata yake ya Ngorongoro na maeneo mengine ikiwamo Irkeepus, Misigiyo, Mokilal, Oloirobi na Kayapus.

Mifuko 1,000 ya chumvi hiyo ilipelekwa Irkeepus na vijiji vingine vilipata mifuko 250 kila kimoja.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Mwangwala alifika eneo la tukio katika Ofisi ya Kijiji cha Kayapus akiambatana na Kaimu Mhifadhi, Needpeace Wambuya, Meneja wa Huduma za Uhifadhi, Elibariki Bajuta, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ngorongoro, Justus Mway na wataalamu kutoka NCAA ambao ni Kilasi Mollel na Cosmas Soombe kwa ajili ya kushuhudia kuwapo mchanga (mawe na rangi nyekundu) kwenye chumvi iliyoingizwa hifadhini kwa ajili ya madini lishe ya mifugo.

Mkuu wa Wilaya baada ya kujionea hali ilivyo, aliagiza kuundwa kwa timu ya wataalamu ndani ya siku saba ili kuleta taarifa kuhusu mambo yanayolalamikiwa ambapo timu hiyo iliundwa na wataalamu kutoka NCAA, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na kutoka baraza la wafugaji kwenda eneo la tukio kwa ajili ya kufanya uchunguzi na ufuatiliaji wa haraka kuhusiana na malalamiko hayo.

Baada ya wataalamu kufika eneo la tukio, timu ilifanya uchunguzi wa awali wa chumvi na hatimaye kuchukua sampuli kutoka katika vijiji mbalimbali kwa ajili ya uchunguzi wa kina wa kimaabara.

Sampuli zilizochukuliwa zilipelekwa Maabara za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dar es Salaam, TBS, Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) Morogoro na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kwa ajili ya uchunguzi wa kina wa uwapo wa mchanga, mawe na rangi nyekundu kwenye chumvi hiyo.

Timu iliyoundwa na Mkuu wa Wilaya kupeleka chumvi maaabara na kufanya ufuatiliaji na kutoa ripoti iliongozwa na

Ofisa Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Ngorongoro, Dk. Chobi Chubwa.

Wataalam wengine ni: Kaayenye Samson Laizer, Ofisa Mifugo na Mkaguzi wa Vyakula vya Mifugo Wilaya ya Ngorongoro; Kilasi Mollel, Ofisa Mifugo NCAA; Simon Saitoti, Diwani wa Ngorongoro na Mwakilishi wa Baraza la Wafugaji.

**UCHUNGUZI WA AWALI**


Uchunguzi wa awali wa uwapo wa mchanga, mawe na rangi nyekundu kwenye chumvi ulianza kwa timu kufanya mahojiano ya moja kwa moja na msambazaji wa chumvi, Idara ya Ununuzi ya NCAA na Idara ya Maendeleo ya Jamii na kubaini mambo kadhaa.

Mambo hayo ni pamoja na zabuni iliyotangazwa na NCAA kuhusu ununuzi wa chumvi nyekundu kutoka Loliondo yenye namba AE/055/2020-2021/HQ/G/15.

Vilevile, mmiliki wa kampuni inayoitwa PANGA BUILDING COMPANY LTD, Marco Panga, alikiri kufanya biashara ya kuuza chumvi ya mifugo aina ya Naju Feed Stock Lick kutoka Nakuru, Kenya kwa NCAA.

Mmiliki wa kampuni hiyo, Panga alieleza kuwa baada ya kupata zabuni ya kununua chumvi, aliagiza chumvi nyekundu ya mifuko miwili kutoka Loliondo kwa mzee Joseph Domel na kuipeleka maabara ya Atomic kwa ajili kupata vibali vya kuingiza chumvi nchini.

Kiasi cha chumvi kilichoagizwa ni mifuko 2,000 yenye ujazo wa Kilo 20 kila mmoja ambayo kwa jumla ni sawa na tani 40 za chumvi yenye thamani ya Sh. milioni 40.



Sehemu ya mifugo na wanyamapori ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. **PICHA: MAKTABA**

# Neema ajira mgodi ukianza uzalishaji

**Na Mwandishi Wetu, IKUNGI**

MGODI wa kati wa uchimbaji wa dhahabu wa Shanta Singida unatarajiwa kuanza rasmi uzalishaji mwanzoni mwa mwaka 2023 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya mgodi huo.

Meneja Mkuu wa mradi huo, Jiten Divecha, alibainisha hayo juzi kwa Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alipotembelea na kukagua Maendeleo ya Mradi wa Mgodi wa Kati wa Dhababu wa Singida (Singida Gold Mine) unaomilikiwa na Shanta Mining Company Limited ulioko Wilaya ya Ikungi mkoani Singida.

Divecha alisema kwa sasa mgodi umeendelea kutoa fursa mbalimbali za ajira kwa Watanzania pamoja na kununua bidhaa za Kitanzania.

Akizungumza baada ya kukagua maeneo ya uchimbaji katika mgodi huo, Dk. Kiruswa aliuagiza uongozi kuhakikisha unamaliza shida zote zinazokwamisha kuanza kwa mradi huo ili uchimbaji uanze.

Alisema wananchi wa Ikungi na wakazi wa Singida wanatarajia kuona mgodi huo unaanza kazi ili wanufaike na uwapo wa mgodi katika jamii yao.

Dk. Kiruswa pia aliipongeza kampuni hiyo kwa uwekezaji mkubwa inaoendelea kuufanya katika mgodi huo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya mgodi, ajira zinazotolewa, afya na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Vilevile, Dk. Kiruswa aliuagiza mgodi wa Shanta kuandaa na kutekeleza mpango wa uchangiaji wa kampuni yao kwenye jamii (CSR) kwa mujibu wa sheria.

Alisema wanatakiwa kuhakikisha kama wawekezaji jamii inayowazunguka inanufaika na mradi husika huku akifurahishwa na Sheria ya Local Content inavyotekelezwa na mgodi huo.

"Nimefurahishwa na mpango wa Local Content, nimetembea hapa sijaona hata mgeni mmoja, wanaofanya kazi hapa wote ni Watanzania, lakini pia mnatumia rasilimali zinazopatikana hapahapa, nimesikia hata maharage yanatoka hapa," alipongeza Dk. Kiruswa.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alimweleza Dk. Kiruswa kuwa wananchi wa Singida wanatamani mradi huo uanze mara moja ili wanufaike na mradi huo.

Alisema mradi utakapoanza utaleta maendeleo kwa jamii inayozunguka pamoja na kuongeza mapato kwa serikali.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri alifuatana na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Ikungi, viongozi wa vijiji na kata wanaozunguka eneo la mradi na wadau wa sekta ya madini.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa wa Tanga, Seleman Mzee Seleman, akizungumza na viongozi wa chama hicho, wilayani Mkinga jana, baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa ofisi mpya ya CCM ya wilaya hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Filamu ya Royal Tour kuzinduliwa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, leo anatarajiwa kuzindua filamu ya Tanzania The Royal Tour mkoani Dodoma na kunadi fursa zilizopo.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia uzinduzi huo na unafanyika leo katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete.

"Kwa Dodoma uzinduzi huu utakuwa wa tofauti, kutakuwa na usiku wa Royal Tour kwenye viwanja na Ukumbi wa Jakaya Kikwete, kutakuwa na mgeni rasmi ambaye ni Makamu wa Rais lakini uongozi wa mkoa umealika wabunge ili kushiriki shughuli hiyo," alisema.

Mtaka alisema kwenye uzinduzi huo itatolewa nafasi kwa sekta binafsi kuzungumzia fursa ambazo Mkoa wa Dodoma utanufaika nazo. "Hatua hii itaonyesha fursa zilizopo Makao Makuu ya Nchi, kutakuwa na burudani itakayobebwa na utamaduni wa kigogo na kirangi na tumetoa fursa kwa wanaofanya shughuli za nyama choma, pia wazalishaji wa mvinyo watapata nafasi,"alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema kutakuwa na shuhuda namna wafanyabiashara walivyopokea fursa za filamu hiyo na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kushuhudia jambo hilo ambalo Rais Samia Suluhu Hassan amelifanya katika kukuza sekta ya utalii na kufungua milango ya sekta binafsi.

Kwa mujibu wa Rais Samia, waandaaji wa filamu hiyo wamelipwa Sh. bilioni saba kwa ajili ya gharama za uandaaji.

## Tigo, Benki Azania waja na Bustisha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano Tigo imeshirikiana na Benki ya Azania kuzindua bidhaa mpya inayoitwa Bustisha kwa lengo la kuwawezesha wateja wa Tigo Pesa kukamilisha miamala yao hata kama hawana fedha za kutosha.

Wateja wanaofanya kazi na Tigo Pesa watastahiki kupata bidhaa hiyo lakini watalazimika kwanza kujisajili na kupata kibali kupitia menyu ya Tigo Pesa au Programu ya Tigo Pesa.

Wateja wanatarajiwa kurejesha malipo ya ziada waliyoongezewa baada ya kuweka au kupokea pesa kwenye akaunti zao za Tigo Pesa.

Akizungumza katika uzinduzi huo juzi jijini Dar es Salaam, Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema: "Tunafuraha kuhuisha bidhaa yetu ya kidijitali ya kibunifu kwa kushirikiana na Benki ya Azania ili kuwapa wateja wetu hai wa Tigo Pesa urahisi wa kufanya miamala zaidi kupitia akaunti zao za Tigo Pesa hata kama hawana salio la kutosha.

"Tunaamini kwamba huduma hii itawapa wateja wetu urahisi wa kufanya miamala bila kizuizi chochote wakati wa mahitaji. Mteja atatakiwa kurejesha ziada aliyoongezewa ikiwa ni pamoja na riba inayotumika kiotomatiki baada ya kuweka au kupokea pesa kwenye akaunti yake ya Tigo Pesa.

"Mteja anaweza kulipa kwa urahisi kupitia menyu ya Tigo Pesa au Programu ya Tigo Pesa na kisha kukatwa moja kwa moja kwenye akaunti yake ya Tigo Pesa ili kurejesha salio lililobaki."

Akizungumza kwa niaba ya Benki ya Azania, Meneja Mwandamizi Hazina, Masoko ya Hisa na Mitaji wa benki hiyo, Rukwaro Senkoro, alisema ushirikiano wa kimkakati wa Benki ya Azania na Tigo kwa ajili ya kuanzisha bidhaa ya Bustisha utaongeza zaidi ushindani katika nafasi ya ukopeshaji wa kidijitali. Alisema bidhaa itampatia mteja anayefanya kazi wa Tigo Pesa huduma ya mkopo ambayo itatozwa ada ya kufikia ya kiasi kilichokopwa na riba ya kila siku kwenye salio lililosalia kulingana na gharama zao za mkopo.

"Wakati unapokuwa na suluhisho rahisi na salama la malipo, ujumuishaji wa kifedha unafuata. Kupitia ushirikiano wetu na Tigo, benki inaweza kutimiza zaidi lengo lake la kusaidia ushirikishwaji wa kifedha na kuwawezesha Watanzania kwa kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma za kifedha," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Aliyosema Samia kuhusu watetezi wa haki sahihi

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya miaka 10 ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu yaliyofanyika Dar es Salaam huku akizungumza mambo mengi kuhusu wanaharakati hao na ushiriki wao katika masuala ya maendeleo ya taifa.

Miongoni mwa mambo aliyoyasema ni watetezi hao kuacha dhana kwamba kuwapo kwao ni kupambana na serikali juu ya mambo mbalimbali na kuwataka kuachana na jambo hilo badala yake waungane na kufanya kazi kwa pamoja. Pia aliwataka kuacha kutetea haki za wanasiasa tu na badala yake wageukie makundi mengine yanayohitaji utetezi, wakiwamo watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili na wanaopoteza maisha kwa ajali za barabarani.

Pamoja na kuwataka kuachana na fikra za kimapambano na misuguano, hakuwakataza kuendeleza uanaharakati wao bali wawe na fikra chanya kwa lengo la kusukuma gurudumu la maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuwa serikali yake haitaki mapambano bali kuwaletea wananchi maendeleo.

Kutokana na mtazamo wake huo, licha ya kutetea makundi maalumu kupata haki zao, aliwataka pia watetezi hao wa haki za binadamu wajenge mfumo wa mazungumzo na taasisi mbalimbali vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama ili kutafuta njia nzuri ya kutatua matatizo ya jamii ikiwamo unyanyasaji dhidi ya raia. Kadhalika, aliwataka watafute fursa ya kukutana naye na kuzungumzia masuala ya haki.


Kauli hizo za Rais Samia zimeonyesha dhahiri kwamba maono yake ndani ya serikali anayoiongoza ni kujenga nchi yenye umoja na mshikamano huku amani ikitamalaki pamoja na kuhakikisha wananchi wanapata haki zao na vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji ambavyo hivi karibuni vimeshika kasi, vinakomeshwa. Ni wazi kwamba mahali popote penye mapambano na misuguano kwa lengo la kuonyeshana umwamba, huwa hakuna maendeleo kamwe. Kwa mantiki hiyo, ni wakati sasa kwa wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu, kuwa na mtazamo chanya katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii. Kama kuna jambo ambalo wanaona linakwenda kinyume cha haki za binadamu, watengeneze ajenda ambayo itatatua tatizo hilo na hatimaye kuwapo kwa hali ya maelewano.

Katika jamii ya kitanzania, kuna mambo ambayo yanasababisha watu katika baadhi ya maeneo kunyimwa haki zao au kunyanyaswa ikiwamo mauaji ya wazee na watu wenye ualbino. Kwa kutumia mifano hiyo, hasa mauaji ya vikongwe, watetezi wa haki za binadamu wanaweza kutengeneza ajenda ya kutungwa kwa sheria ambayo itawezesha wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Miaka ya 1990, kwa mfano, kutokana na kukithiri kwa ubakaji na ulawiti, wanaharakati walianzisha ajenda ya kutungwa kwa sheria ili kukomesha vitendo hivyo na hatimaye kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. Hata sasa kupitia THRDC inawezekana zikaibuliwa ajenda mbalimbali ambazo zitawezesha kupatikana kwa haki za binadamu na kukomesha ukiukwaji wa haki hizo. Mfano wa mambo yanayoweza kuibuliwa na watetezi wa haki na wanaharakati ni wimbi la ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu. Kupitia hoja hiyo, watetezi hao wanaweza kuchambua Sheria ya Usalama Barabarani kuainisha upungufu uliomo na hatimaye kufanyiwa mabadiliko kama vile adhabu ya makosa ya usalama hasa madereva wanaosababisha ajali na hatimaye watu kupoteza maisha.

Wakati umefika sasa kwa wadau wote wa maendeleo, wakiwamo watetezi wa haki za binadamu, kubadili fikra na mtazamo na kujielekeza zaidi katika masuala ya maendeleo. Jambo la msingi ni kufahamu kwamba tunajenga nyumba moja, hivyo hakuna haja ya kugombea na kunyang'anyana fito.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Maridhiano ya kisiasa yanayohimizwa yasibezwe

**NIANZE** kwa kumpongeza Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, kwa hatua mbalimbali anazochukua tangu achaguliwe kushika nafasi hiyo, zenye lengo la kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vya siasa.

Miongoni mwa hatua hizo ni kuwataka viongozi na wanachama wa CCM kuwa tayari kwa maridhiano ya kisiasa aliyoyaanzisha Rais Samia kati ya chama hicho tawala na vyama vyote vya siasa.

Komredi Kinana ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, ameonyesha mfano wa mzuri na wa kuigwa kwa kuanzisha mchakato huo kwa kukutana na vyama na taasisi mbalimbali za kisiasa.

Anataja mambo manne anayoshughulikia kuwa ni maridhiano, kuvumiliana, mabadiliko kwenye taasisi na kulijenga upya taifa, kwa kuwa Tanzania ni ya vyama vingi vya siasa, hivyo kuwapo kwa maridhiano ni jambo muhimu.

Kama nilivyoanza kuelezea, ninampongeza kwa hatua hiyo, kwani ni ukweli kwamba siasa si uadui, hivyo ni wazi hakuna sababu ya msingi ya kugombana wenyewe kwa wenyewe kama vyama au kugombana na chama tawala.

Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, alianzisha maridhiano kati ya CCM na vyama vyote vya siasa, hivyo Komredi Kinana anasema hana budi kuendeleza maridhiano hayo.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, mazungumzo ya wanasiasa yanajenga maridhiano yatakayoweka mazingira bora ya kuendeleza amani na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mazungumzo yanayolenga kufungua ukurasa mpya wa siasa nchini, yangekuwa ni malengo ya kika mwanasiasa ili kile ambacho Kinana anakitangaza kiweze kuzaa matunda na kuwa siasa za kupingana kwa hoja.

Lakini pia ninaomba nikumbushe wanasiasa kuwa kuna maisha baada ya siasa, hivyo si vyema kuchukiana kwa sababu ya siasa, ikizingatiwa kama mtindo huo ukatupwa mbali na kuacha maridhiano yachukue nafasi.

Pamoja na hayo, uadui katika siasa ungebaki katika majukwaa ya kampeni, lakini baada ya hapo wanasiasa wabaki kuwa wamoja, wanaojadiliana kuhusu maendeleo ya taifa lao bila kujali itikadi za vyama vyao.

Ikumbukwe kuwa Rais Samia amekuwa akisisitiza kila mara kuwa Tanzania haitajengwa na chama kimoja, na kwamba ni lazima kuwe na ushirikiano, na kuwataka Watanzania wote kushiriki kujenga nchi yao kwa misingi iliyo sawa.

Mbali na hilo, anagusia kuwa vyama vya siasa vinao umuhimu mkubwa katika kuangalia na kukosoa yale yanayoendelea katika serikali na kutoa maoni ili kuirekebisha serikali iliyoko madarakani.

Katika mazingira hayo, ni wazi kwamba yapo matumaini ya baadaye ya uwapo wa siasa na demokrasia inayoshamiri ambayo Rais anaamini kuwa ndiyo ambayo Watanzania wanaitaka.

Lakini pia ingekuwa vyema kama Baraza la Vyama vya Siasa kuhakikisha linatimiza wajibu wake inavyotakiwa, ikiwamo kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa juu ya migogoro inayotokea katika vyama vya siasa.

Kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa juu ya masuala yenye maslahi kwa taifa kuhusiana na vyama vya siasa au kuhusiana na hali ya kisiasa nchini ili kuhakikisha zinapotokea tofauti, maridhiano yachukue nafasi.

Ninashauri hivyo kwani Baraza la Vyama vya Siasa linaundwa ndani ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, huku wajumbe wake wakijumuisha viongozi wa kitaifa wawili wa kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Mafanikio ya TARURA, yameibeba TAMISEMI na kumng'arisha Samia



Na Pascal Mayalla

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Innocent Bashungwa, wakati akilishukuru bunge kupitisha makadirio ya mapato na matumizi OR-TAMISEMI, kwa mwaka wa Fedha 2022/23 baada ya kuidhinishiwa Sh. trilioni 8.779, alimshukuru Rais Samia kuongeza bajeti ya TARURA kwa karibu mara tatu.**

MAFANIKIO ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) yameendelea kuibeba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), huku yakizidi kumng'arisha Rais Samia Suluhu Hassan ndani ya mwaka wake huu mmoja madarakani.

Hayo yamebainishwa katika makala maalum ya kuzungumzia mafanikio ya TARURA ndani ya mwaka mmoja wa serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia. Kwa kuanzia, Rais Samia amepongezwa kwa kuongeza bajeti ya TARURA kwa karibu mara tatu.

Mafanikio hayo ya TARURA na jinsi yalivyoibeba TAMISEMI na kumng'arisha Rais Samia, yamejidhihirisha wazi hata katika mijadala na majadiliano Bungeni katika vikao vya Bunge la Bajeti vinavyoendelea jijini Dodoma, kwa wabunge wengi kuipongeza kazi nzuri inayofanywa na TARURA, kuzifungua barabara za vijijini na mijini ni kuifungua nchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Innocent Bashungwa, wakati akilishukuru bunge kupitisha makadirio ya mapato na matumizi OR-TAMISEMI, kwa mwaka wa Fedha 2022/23 baada ya kuidhinishiwa Sh. trilioni 8.779, alimshukuru Rais Samia kuongeza bajeti ya TARURA kwa karibu mara tatu.

Alisema huko mitaani Rais Samia anasemwa anaupiga mwingi, hivyo Waziri Bashungwa ameahidi TAMISEMI kama sehemu ya TARURA, kuunda kikosi kazi cha timu ya ushindi na yeye (Bashungwa) kwa niaba ya timu hiyo ya ushindi ya TAMISEMI, amemshukuru Rais Samia. Alisema wazi kwamba wanamuunga mkono na kumhakikishia Rais kusimamia kikamilifu ili aendelee kuupiga mwingi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, amesema mafanikio ya TARURA ikiwa moja ya taasisi saba chini ya TAMISEMI, yameitoa kidedea TAMISEMI kwa kuwa kila unapopita, unashuhudia kazi nzuri ya TAMISEMI katika kuifungua nchi. Ameupongeza uongozi wa TARURA, kuanzia Bodi ya Uongozi, menejiment na wafanyakazi kwa kufanya kazi kwa bidii, kujituma na kwa weledi wa hali ya juu kutimiza malengo tarajiwa.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, amesema taasisi hiyo ilianza rasmi Julai 2, 2017 kwa lengo la kutoa matengenezo endelevu na gharama nafuu na maendeleo ya mtandao wa barabara vijijini na mijini ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii nchini Tanzania.

Anabainisha kuwa dira ya TARURA ni kuwa taasisi inayoongoza katika menejimenti ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini huku dhima yake ikiwa ni kupanga, usanifu, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kuzingatia ufanisi wa gharama kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Lengo la kuanzishwa kwa TARURA kulitokana na changamoto zilizokuwapo za hali ya miundombinu ya barabara mijini na vijijini.

Kwa hiyo TARURA ilianzishwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za mtandao wa barabara za wilaya zenye urefu wa kilomita 144,429.77.

Tangu kuanzishwa kwake, tumeshuhudia wakala ukifanikisha kazi nyingi hususan ufanisi wa malengo sita ya kimkakati na sasa inaendelea na vipaumbele vya kutunza barabari zenye hali nzuri; kuondoa vikwazo kwenye mtandao wa barabara za wilaya, kuhakikisha zinapitika wakati wote; na kupandisha hadhi barabara za udogo kuwa za changarawe, za changarawe kuwa za lami kwa kuzingatia vipaumbele vya kiuchumi na kijamii.

Sambamba na hayo, mikakati mingine ni matumizi ya teknolojia katika utengenezaji wa barabara huku matokeo tarajiwa yakiwa barabara zenye hali nzuri zitakuwa zaidi ya asilimia 50 na mkakati huu wa pili utatumia zaidi ya Sh. trilioni nne.

Kutokana na mafanikio hayo pamoja na Rais kuongeza bajeti ya TARURA, Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi, Mhandisi Florian Kabaka, alimalizia kwa kutoa pongezi kwa bodi, menejimenti na wafanyakazi wa TARURA kwa kufanya kazi kwa bidii kwa moyo na kujituma, kwa miradi kutekelezwa nchi nzima.

Mwenyekiti nae alijiunga na wengine kutoa shukrani kwa Rais Samia akisema ongezeko la bajeti ya TARURA zimeiwezesha TARURA kufanya maajabu makubwa kwa ujenzi wa barabara, na madaraja.

Kwa hayo yanayoendelea TARURA, Rais Samia anaendelea kuupiga mwingi na ni wazi kwamba kwa mtaji huo hali ya barabara itakuwa nzuri na hakutakuwa na kero tena ya barabara wakati wa mvua. Kwa maneno mengine, barabara zetu, iwe masika, iwe kiangazi, zitapitika bila wasiwasi na tutashuhudia hata kero ya usafirishaji wa mazao inatoweka.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kumbe somo la Historia ni fumbo la imani!



Na Joseph Kulangwa

**Kwa kweli huku kuaminishana nako kuna matatizo yake, hebu fikiria mwanafunzi saa tano anakuwa darasani akisoma Historia na kuambiwa binadamu alitokana na sokwe au nyani, lakini saa sita anaingia katika kipindi kingine, cha Dini, anaambiwa binadamu alitokana na Adam na Eva.**

MTOTO mdogo akiwa analia sana ukamtishia kuwa nyau atakung'ata na kweli akasikia mlio wa nyau, atanyamaza hata kama hakuwahi kung'atwa na paka huyo atatii kwa uoga kutokana na kuaminishwa tu.

Uoga ataendelea kuwa nao hata akimwona nyau anapita zake na mambo yake. Hiyo ni imani ambayo kila binadamu huweza kuaminishwa na akaamini kuwa ni kweli. Ni sawa na kuamini kuwa Mungu yupo.

Kuna nyakati huibuka ubishi miongoni mwa jamii kuhusu kuwapo au kutokuwapo Mungu, hivyo kuibuka pande mbili za kiimani na ndipo inaposhindikana, basi watu huambiana bora kuamini Mungu yupo ukaenda mbinguni usimkute, kuliko kutoamini na ukaenda ukamkuta.

Bila kuambiana hivyo, inakuwa songombingo kwa sababu fikiria unajiaminisha Mungu hayupo lakini siku ya siku ukaenda mbinguni kumbe ndiye akakufungulia lango kuu, utajihisi vipi kama si moto!

Tuendelee kuamini uwapo wa Mungu kwa sababu bila hivyo, si rahisi kufikiria jinsi binadamu alivyoumbwa mpaka akawa alivyo leo kutokana na imani kuwa mtu alianzaanzaje au alikujakujaje.

Hilo linanirudisha kwenye hoja aliyoitoa mbunge mmoja bungeni hivi karibuni, akijadili makadirio na mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenye mihutasari itumikayo kufundisha shuleni hususan katika somo la Historia.

Mbunge akahoji sababu ya kuendelea kufundisha somo hilo kwa watoto wakiaminishwa kuwa mtu alitokana na sokwe, kwamba mamilioni ya miaka iliyopita mtu huyu anayeonekana leo, alikuwa sokwe na kidogokidogo akabadilika na kuwa alivyo sasa.

Yaani hivi sasa hana manyoya kama aliyonayo sokwe na anazungumza tofauti na sokwe, na ana uwezo wa kufikiri na kuamua. Mbunge akauliza inakuwaje hivi sasa kuna sokwe na hawabadiliki kuwa watu kulikoni!

Akahoji sana na kutaka kujua kama simba zamani walikuwa mbwa au ng'ombe zamani walikuwa mbuzi, nami nikajiuliza, hivi yawezekana mbwa zamani walikuwa fisi au? Kwa nini mabadiliko haya yahusishe binadamu tu na si wanyama au wadudu?

Kwa kweli huku kuaminishana nako kuna matatizo yake, hebu fikiria mwanafunzi saa tano anakuwa darasani akisoma Historia na kuambiwa binadamu alitokana na sokwe au nyani, lakini saa sita anaingia katika kipindi kingine, cha Dini, anaambiwa binadamu alitokana na Adam na Eva.

Akitoka hapo, saa saba anaingia kipindi cha Biolojia, anaambiwa binadamu alitokana na seli, lakini akifafanuliwa katika somo linalohusu kuzaliana, anaambiwa binadamu ni muunganiko wa mbegu za mwanamume na yai la mwanamke.

Sasa hapo ndipo utakuta wanafunzi wanachanganyikwa wachukue lipi na waache lipi katika kujua chanzo hasa cha binadamu ni nini? Akiingia kwenye mitihani na masomo yanauliza swali hili hili, afanye nini, ingawa atajibu kulingana na muktadha uliopo.

Haya mambo yanatufanya siku nyingine tujiulize kama ni kweli binadamu wa kwanza duniani alitokea Olduvai Gorge, akigundulia na Dk. Leakey, tukionyeshwa fuvu ambalo ukiliangalia sana utaona ni la sokwe.

Utajiuliza ni nani alithibitisha kuwa huyu ndiye mtu wa kwanza duniani? Unaweza kujiuliza je ndiye Adam ambaye katika dini tunaambiwa alipatikana katika Bustani ya Eden huko Mashariki ya Kati? Iweje aibukie Oduvai Gorge?

Ni mambo ya imani tu, na wakati mwingine hayana ushahidi madhubuti lakini yanaletwa kwa msingi wa masomo na kufanya mitihani ili kufaulu, hivyo mwanafunzi kulazimika kuamini, ili asije akafeli mtihani.

Na kimsingi mambo haya mengine yalikuja na dini zilizoletwa na wageni kutulainisha, ili wafanye waliyotaka kuyafanya na ndiyo sababu katika historia hiyo hiyo, tunaambiwa walikuja kwanza wapelelezi kuangalia kuna nini na kinafanyika nini na watu walipo wakoje.

Baada ya kubaini vilivyokuwapo kuwa vitawanufaisha, wakaja Wamisionari na dini zao kutulainisha kwa lugha ya sisi ni wana wa Mungu mmoja tunaostahili kupendana, ili tuwaache wavune wasichopanda kwa majina na maneno matamu yaliyoandikwa na yasiyoandikwa.

Hata hivyo, kwa kuwa tunaamini siku moja tutakwenda mbinguni kama hatutafanya dhambi, basi tuamini hivyo na kwamba tulitoka kwa udongo tutarudi kwa udongo, hata tukizikwa kwenye majeneza ya plastiki zisizooza. Lakini somo la Historia lipunguziwe mada na maudhui, ili tusome yanayotufaa na si njozi na imani.

**Alamsiki!**

# Familia ni msingi wa malezi, utu katika jamii



LEO ni Siku ya Familia Duniani. Wakati siku hii ikiadhimishwa, hivi sasa wanadamu wanaishi katika jamii inayobadilika kwa kasi kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiroho. Mabadiliko haya yanapotokea huambatana na changamoto mbalimbali.

Ziko changamoto nyingi katika jamii na familia nyingi za leo kama vile kukosa upendo na uaminifu, watu kutokuwajibika katika ndoa, magonjwa, kuongezeka kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuongezeka kwa mauaji na vitendo vya ukatili katika familia.

Changamoto zingine ni kuongezeka kwa familia za mzazi mmoja, ongezeko la migogoro na kuvunjika kwa ndoa, vijana wengi kuogopa kuingia katika ndoa, watoto kukosa upendo na malezi bora na usasa na mambo yake. Yote haya huleta matatizo katika familia na jamii.

Katika kuadhimisha siku hii adhimu, jamii inapaswa kutambua kwamba kila binadamu ametoka katika familia. Watu wako jinsi walivyo kwa sababu familia zao zimewatengeneza kwa kuwa tabia na mienendo ya mtu inajengwa katika familia.

Wanasaikolojia wanasema, zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya makuzi na malezi wakati wa utoto. Hii ina maana kwamba ustawi wa jamii na taifa unaanzia nyumbani kwa kuwa uhai wa taifa unategemea uhai wa familia.

Wakati wa kuadhimisha siku hii muhimu, jamii inakumbushwa kuwashukuru wazazi na kuwasaidia katika uzee wao ili kupata neema na baraka mbele za Mwenyezi Mungu kwani bila wao watu wasingekuwapo.

Kadhalika, Siku ya Familia Duniani inamkumbusha kila mwanandoa kumshukuru mwenzi wake kwa upendo anaomwonyesha, mchango wake katika maendeleo ya familia, kwa kumvumilia na kumsamehe alipomkosea. Ni wakati wa familia kupongezana, kujitathmini na kuboresha uhusiano na uwajibikaji.

Kadhalika, watoto wanayo nafasi kubwa katika ustawi wa familia kwa kuwa ni kiungo kikubwa sana cha baba na mama na chanzo cha furaha katika familia. Kwa mantiki hiyo, siku ya familia pia ni siku ya wazazi kumshukuru Mungu kwa zawadi ya watoto aliowajalia kwani watoto wanawapatia uzoefu wa kuitwa baba au mama.

Siku ya familia duniani ni siku ya kuwaombea watoto kwa Mungu dhidi ya maovu na majanga ili wapate mafanikio katika maisha yao na kufanyika baraka kwa jamii na wazazi wenyewe.

Familia inapokosa misingi bora, husababisha watoto kutopata malezi mazuri.

Watoto wasipofunzwa maadili mema na stadi za maisha wakati wa utoto, wakiwa vijana au watu wazima hawataweza kukunjika tena ndiyo maana wahenga walisema "mkunje samaki angali mbichi".

Mtoto ni malezi, hivyo ni wajibu wa baba na mama kuwapa watoto malezi bora. Watoto wanapaswa kurithishwa tunu zilizo njema.

Malezi bora ni ufunguo na urithi wa maisha kwa mtoto. Taasisi, jamii na taifa bora la kesho, linategemea malezi bora yanayotolewa na taifa bora la leo. Malezi bora huanzia katika ngazi ya familia.

Malezi bora ndiyo mwelekeo sahihi wa maisha ya mtoto kwani kesho bora ya mtoto inajengwa na leo bora ya wazazi au walezi bora. Siku zote matunda mema hutoka katika mti bora.

Familia ni msingi na kitengo kinachomtengeneza mtoto kiroho, kimwili na kitabia (attitudes). Vitengo vingine kama taasisi za dini au shule husaidia tu na kuendeleza msingi uliojengwa na wazazi au walezi.

**Watu wako jinsi walivyo kwa sababu familia zao zimewatengeneza kwa kuwa tabia na mienendo ya mtu inajengwa katika familia... zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya makuzi na malezi wakati wa utoto.**

Kazi ya vitengo vingine inaweza kuwa nyepesi au ngumu kutegemea na jinsi kitengo cha msingi yaani familia kilivyotekeleza jukumu lake la malezi.

### VIONGOZI WA KESHO

Watoto wa leo ni raia na viongozi wa kesho; ndio watakaokuwa na sifa au aibu kwa wazazi wao, kwa familia zao, kwa jamaa na taifa lao.

Kwa hiyo, wazazi au walezi wanapaswa kuwa mfano bora wa kauli, matendo na mienendo yao kwa watoto.

Familia ni kitovu cha malezi, utu na shule ya kutambua mapenzi ya Mungu.

Watoto wenye malezi bora; walioelimishwa kumcha Mungu watakuwa na utii, upendo, na msaada mkubwa kwa wazazi wao katika umaskini na uzee wao na kufanyika baraka kwa watu wengine pia.

Ni dhahiri kuwa jukumu la kujenga jamii na taifa au kuliboмоa, wanalo wazazi au walezi. Kwa hiyo, suala la malezi katika ngazi ya familia ni ajenda muhimu katika jitihada za kukabiliana na mauaji na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika familia na matendo yote maovu katika jamii ili kupata suluhisho la kudumu.

Wanandoa wanapaswa kuishi kwa ushirikiano na kila mmoja atimize majukumu yake katika familia. Kila mmoja anastahili heshima, haki na kuthaminiwa, hivyo ni wajibu wa kila mzazi au mlezi kuifanya nyumba na familia yake kuwa mahali pa sala, furaha, starehe na makao ya Mungu. Familia zinapaswa kumwomba Mungu ili azibariki ziwe chimbuko la taifa lenye ustawi, amani na maadili mema.

■ **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.1.**

# MAISHA

MEI 15, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

**Kuwa Kiafrika zaidi**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Fahamu sababu zinazochangia nyumba kuvuja



Ukurasa 12

**HARUSI**




**KUCHA NYEUPE**


# Tumia njia hizi utatabasamu

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M | K | U | K | I |
| | S | | | I | |
| D | O | A | | M | |
| | N | | T | B | C |
| | D | | | I | |
| D | O | N | D | A | |




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
TUA, AMA, MAMBA, TEMBO, BABUKA, TAMBUA

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa nyumbani na bibi yake akisimuliwa hadhithi za zamani. Wakati akisikiliza hadithi macho yake yalikuwa yakimwangalia bibi yake usoni huku akiwa na sura ya kuogopa.

Bibi yake aligundua Juma amepata hofu na hadithi aliyokuwa akimsimulia, alimgeukia na kumuuliza.

**Bibi:** Juma mjukuu wangu mbona unanitazama sana?

**Juma:** Bibi naogopa hadhithi za mazimwi, japo mwalimu alituambia ya kale ni dhahabu, lakini hadithi hizi siwezi kuhimili.

**Bibi:** Mwalimu wako yuko sahihi kwani anakuhimiza uthamini utamaduni wako na kukumbuka ulipotoka na ndio maana ya msemo huo.

**Juma:** Sawa bibi kuanzia sasa sitaogopa, nitasikiliza na kuthamini utamaduni wetu.

**SWALI**
Dau na Ngalawa tofauti zake ni nini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Zijue sababu zinazofanya watu kukata tamaa

***KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo.***

Leo hebu tujadili kuhusu na jinsi kunavyotesa watu wengi katika kufikia hatma yao ya mafanikio katika maisha.

Kukata tamaa ni dhambi kwa sababu ni kama vile unamwambia Mungu kwamba humwamini tena kwa kuwa ameshindwa kukufanikisha. Mungu mwenyewe katika moja ya maandiko yake anasema, “Imewapasa kumuomba Mungu siku zote, wala msikate tamaa”.

Mtu anayekata tamaa anaangalia mazingira au matokeo ya jambo alilofanya na kuamua kuwa haiwezekani tena kuendelea mbele. Roho yake inashuka, nguvu zinamwishia na hatimaye machozi humdondoka anakubali kushindwa.

Mara nyingi aliyekata tamaa hulaumu na kumchukia karibu kila mtu, akiwaona kama ndio sababu ya kushindwa kwake.

Kamwe hajiangalii mwenyewe na kuona wapi alikosea, bali ataona ameonewa, amedhulumiwa na Mungu anamwacha.

Kilele cha mtu aliyekata tamaa ni kujitenga na jamii na hali hii isiporekebishwa hupelekea hata kujiua! Mtu aliyekata tamaa humfungulia shetani mlango pengine pasipo kutambua.

Shetani atatumia watu kukuonyesha jinsi ambavyo huwezi kufanikiwa, atakukumbusha na kukuonyesha mambo uliyoyashindwa! Kwa sababu kukata tamaa kuna wasilishwa na roho ya kutomtumaini Mungu, unajikuta unaanza kutafuta msaada nje ya Mungu.

Mwanafalsafa mmoja, Steve Jobs, akizungumzia dawa ya kutokata tamaa alisema; “Kama hujaiona bado, endelea kutafuta usiache....”. Ukianguka jitahidi kuinuka, kama huwezi kuinuka tambaa, lakini usikubali kubakia hapo hapo ulipoangukia!

Mtu aliyekata tamaa anapoanguka hafanyi jitihada ya kuinuka, atabakia hapo alipo na kuwalaumu watu wengine kwa nini hawamwinui. Wiston Churchill akizungumzia wakataji tamaa alisema; “ Huyu huona ugumu katika kila fursa, mwenye matumaini huona fursa katika kila ugumu”.

Msomaji wangu, baada ya utangulizi huo, hebu sasa tuangalie sababu zinazofanya watu wengi kukata tamaa pale wanapofukuzia mafanikio katika maisha yao.

Moja ya sababu ni kutarajia mafanikio ya haraka. Wapo watu wanaotarajia kupanda leo na kuvuna kesho, hawana roho ya subira. Wanashindwa kuelewa kwamba uvumilivu ni tunda la roho na ni nguzo kuu ya mafanikio!

Unapoona jambo utakalo kulifanya litachukua muda mrefu unaachana nalo, wenzako wanalifanya na kwa uvumilivu mwingi na wakati ukifika wanafanikiwa. Wewe unakuwa umebaki pale pale bila kujiongezea lolote. Ufanye au usifanye lolote, muda utakuja na kukupita na kukuacha ukibaki kulaumu kila kitu.

Yupo mtu anaona kwenda chuo kusoma miaka mitatu ni mingi sana, au kuwekeza katika upandaji miti inachukua muda mrefu. Asilojua ni hili, kwamba hiyo miaka anayoiona kwamba ni mingi itakuja na kupita na wale walioenda chuo watamaliza na kurudi yeye akiwa vile vile.

Kile kinachopatikana kwa haraka huisha kwa haraka, fumba na kufumbua kimetoweka. Ipo tofauti kati ya malengo ya muda mfupi na tamaa ya mafanikio ya haraka! Malengo ya muda mfupi yanahasilishwa na hali halisi na hupangiliwa kwa makini.

Mafanikio ya haraka ni kutamani upate leo hata kama lengo hilo mafanikio yake yatakuja baada ya muda mrefu. Mwenye kutaka mafanikio ya haraka hapangilii vema yale anayotaka kufanya, anaamini katika kupiga ‘dili’. Tabia hii ya kutaka mafanikio kwa njia ya mkato imeleta maafa, maumivu na majuto kwa wengi.

Mungu mwenyewe ameweka bayana kwamba hakuna njia ya mkato katika kupata mafanikio pale aliposema kwenye maandiko yake kwamba; “Mali iliyopatikana kwa haraka, itapunguka; bali yeye achumaye kidogo kidogo atazidishiwa”. Pia akasema, “Mtu mwaminifu atakuwa na baraka tele; Lakini afanyaye haraka kuwa tajiri hakosi ataadhibiwa”.

Aliko Dangote, raia wa Nigeria, mwaka 2008 alitajwa kuwa tajiri mkubwa kuliko watu wote weusi Afrika. Je, yeye anasemaje kuhusu kupata mafanikio haraka haraka?

“Niliunda makampuni na kutokea kuwa tajiri mkubwa Afrika, lakini haya hayakutokea kwa usiku moja! Imenichukua miaka 30 kufikia hapa nilipo leo”!

“Vijana wa leo wanatamani kuwa kama mimi, lakini wanataka mafanikio haya kwa usiku mmoja. Hautafanikiwa. Kujenga biashara yenye mafanikio, anza kidogo ukiwa na ndoto kubwa. Katika safari ya ujasiriamali kushikilia lengo lako ni muhimu sana”, anasema Dangote.

***Msomaji wangu, Leo tuishie hapa, tutaendelea wiki ijayo, Je, una maoni? Tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# ATCL itumie vyema ndege zake kutangaza vivutio vyetu

MOJA ya mbinu zinazotumiwa na mataifa mengi duniani kutangaza utalii ni kuweka majarida yenye maelezo ya kutoa sababu kwa nini mtalii aone Tanzania ndiyo eneo la kutembelea na kutumia fedha zake anapohitaji kupumzika.

Mathalani, nimewahi kusafiri kwenda Geneva na ndege ya Shirika la Ndege la Uturuki (Turkish Airlines) nikakuta jarida lenye vivutio vya utalii duniani, vyote vinalenga kumfanya mtu aone kwa nini anapaswa kutenga muda kutembelea vivutio mbalimbali.

Ndani ya jarida hilo, nilikuta makala mbalimbali zilizoandikwa kwa ustadi mkubwa wa kuuza bidhaa ya utalii na nchi jirani ilikuwa na kurasa kadhaa za kutangaza vivutio mbalimbali.

Pia wiki hiyo katika jiji hilo la kitajiri la Geneva, magari, treni na mabango yalipambwa na picha za vivutio na kuonyesha kwa nini mgeni apange safari ya kwenda nchini humo na kutumia siku nyingi.

Kwenye ndege za ndani za shirika la ndege za nchi hiyo (jina limehifadhiwa) zinazofanya safari za ndani na nje ya nchi, kuna jarida la kumwezesha mtu kusoma kuongeza maarifa, lakini zaidi kutengeneza sababu kwanini atembelee nchi hiyo.

Mathalani, mgeni anayesafiri kutoka nchi hiyo kwenda Afrika Kusini anatumia saa nne angani, maana yake atahitaji kusoma akikuta kijarida cha kumpa maarifa,na hata kama alishapanga safari yake kwenda kutalii, itamshawishi wakati mwingine kufanya hivyo.

Jitihada nyingi zimefanyika kutangaza utalii wa Tanzania, ikiwamo hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aliporekodi filamu ya The Royal Tour, iliyolenga kutangaza vivutio vilivyoko nchini kwa masoko ya utalii duniani, kubwa likilengwa la Marekani.

Kwa sasa serikali inaendelea na jitihada za kueleza kwanini filamu hiyo ilitengenezwa na kwa namna gani inakwenda kuleta mafanikio kwa kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo rasmi, kuchangia ukuaji wa uchumi na kubadilisha maisha ya mtu mmoja mmoja.

Pia uzinduzi wa filamu hiyo kwenye mikoa ya Arusha, Zanzibar na Dar es Salaam baada ya kuzinduliwa kwa mara ya kwanza Marekani, umekusudia kuleta wageni zaidi nchini ili kukuza uchumi wa nchi.

Wakati haya yakifanyika, kuna jambo ambalo ni muhimu kufanyika na mara zote niliposafiri nimejiuliza kwa nini halifanyiki na kama kuna vikwazo ni jitihada gani zimefanyika kuviondoa.

Mara kadhaa nimesafiri na Ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) za aina zote kwa safari za ndani na nje ya nchi kama kwenda Zimbabwe na Zambia ambazo ni safari za muda mrefu wa zaidi ya saa sita.

Msafiri anapokwenda Zambia ndege huondoka Dar Es Salaam na kwenda hadi Zimbabwe ambako hubeba wasafiri wengine wanaoenda Tanzania, inatua Zambia inashusha abiria na kupakia wengine, mwisho wa safari huwa ilikoanzia.

Ndani ya nchi tuna safari nyingi za mikoa mingi na nimefanikiwa kusafiri kwenye safari zote na kila nilivyosafiri nilitafuta kijarida au kitu cha kujisomea kilichowekwa ndani ya ndege sikukikuta.

Inavyoonekana tumeshindwa kutumia uwapo wa ndege zetu kuwa na jarida linaloelezea mambo ya nchi yetu kinagaubaga, kwamba mgeni aliyekuja nchini kwa sababu za kibiashara aone umuhimu wa kutembelea vivutio vya utalii.

Mathalani, ndege inayokwenda Dodoma hubeba wawekezaji na wageni wengine wanaokwenda kukutana na viongozi wa serikali. Dakika 45 wanazokuwa ndani ya ndege zinawatosha kusoma na kutengeneza sababu ya kuzialika familia au jamaa zao walioko mbali kuja kuitembelea nchi yetu.

> **“Kwa sasa tuna viwanja vya ndege vilivyokarabatiwa ila bado havijaweka matangazo ya utalii, mathalani Dodoma, Mwanza, Mtwara na kwingine ambako tunaweza kutangaza na kutengeneza sababu ya mgeni kuja kwetu.**

Ninaamini lazima kuwa na mkakati endelevu wa kutangaza vivutio vyetu bila kuchoka,kwamba mtu akiwa kwenye uwanja wetu iwe ni Terminal I,II au III aone sababu ya kutumia fedha zake nchini.

Kwamba uwanjani akaribishwe na picha za bidhaa zetu, akiingia kwenye ndege akute jarida lenye maelezo ya kutosha na anaposhuka uwanja mwingine akutane na matangazo ya kumjengea matamanio ya kusafiri zaidi.

Kwa sasa tuna viwanja vya ndege vilivyokarabatiwa ila bado havijaweka matangazo ya utalii,mathalani Dodoma, Mwanza, Mtwara na kwingine ambako tunaweza kutangaza na kutengeneza sababu ya mgeni kuja kwetu.


Ni muhimu jitihada zote zikaenda sambamba ili kuongoza idadi ya watalii nchini, nguvu kubwa imewekwa kwenye Royal Tour ni sawa kabisa,lakini hata matangazo kwenye mashirika yetu ya ndege ya ndani na wenzetu ni muhimu sana.

Nimezungumzia ATCL kwa kuwa ni mali ya Watanzania lakini yako mengine binafsi ambayo nilibahatika kusafiri nayo hayana majarida yoyote ya kueleza vivutio vyetu, naamini usipojisemea hakuna wa kukusemea,ni muhimu tuanze sasa au turejeshe utaratibu huo.

# HARUSI













Bwana na Bibi Mzunguwanzala wakifurahia jubilee ya miaka 35 ya ndoa, katika ibada maalum ya kuwabariki iliyofanyika katika Kanisa la Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu, Kitunda Jijini Dar es Saalam jana.

# MITINDO








## Kuwa Kiafrika zaidi

MAVAZI na mapambo ya asili ya Kiafrika imepata umaarufu hapa nchini kutokana na umaridadi wake.

Wanawake na Wanaume wamekuwa wafuasi wa aina hii ya mavazi ambayo awali ilionekana kama ni mitindo ya kizamani iliyopitwa na wakati.

Wabunifu wameongeza chachu ya mavazi hayo kutokana na kunogesha kwa mitindo ya kisasa iliyonakshiwa na aina nyingine za nguo.

Kutokana na hali hiyo watu wengi wamebuni njia tofauti za kuyafanya mavazi hayo yawe ya kutokea katika shughuli mbalimbali za kijamii pamoja na ofisini.

**JINSI YA KUTUMIA**

Nguo zenye rangi ya bluu, nyekundu na zambarau ambazo zinaakisi makabila mengi ya kiafrika, zinatumika kutambulisha uasili wa jamii zetu.

Magauni, mashati na suruali zinazotengenezwa na kuvaliwa katika mitindo ya asili inampa mvuto zaidi mtumiaji na kujiamini.

**Mtandio**

Nguo maalum inayotumika kama mgolole yenye rangi mchanganyiko, kwa sasa inatumika kama mitandio au kuvaliwa kama kilemba.

**Bangili**

Bangili za shanga ni moja ya mapambo ambayo watu wanapenda kutumia kuvaa mikononi mwao kila siku. Ni jambo la kawaida kuona kwenye sherehe mbalimbali wamevaa bangili hizo kuanzia shingoni hadi mikononi.

**Viatu**

Mitindo ya viatu inayoendana na jamii zetu imekuwa kawaida siku hizi, mfano viatu vyenye nakshi za shanga na vile vilivyotengenezwa kwa kutumia tairi za gari vimependa soko baada ya watu wengi kupenda kuvitumia.

UREMBO





KUCHA NYEUPE

# Tumia njia hizi utatabasamu

WANAWAKE wengi wamekuwa wakiharibu kucha kwa kupoteza rangi yake ya asili kwa matumizi ya rangi bandia.

Leo nitakuletea njia ya kurudisha rangi asili ya kucha zako zilizofubaa kutokana na matumizi ya vipodozi. Sio lazima uende kusuguliwa saluni, kaa nyumbani kwako fanya mwenyewe njia hizi utaona matokeo mazuri.

**Mahitaji**

Mahitaji yanayoweza kukusaidia kurejesha weupe wa asili wa kucha zako zilizofubaa ni dawa ya mswaki na Baking soda.

**Jinsi ya kusafisha kucha**

Chukua dawa ya mswaki changanya na unga wa Baking soda kisha weka kwenye kucha zako.

Sugua na mswaki mpaka uone uchafu unatoka ukisharizika kwa kuona zimetakata unaweza kunawa na sabuni na maji masafi.

Ukimaliza futa kucha na vidole vyako kwa taulo safi na kisha paka losheni yako kama kawaida.

**Limao na Baking Soda**

Kadhalika unaweza kutumia limao na baking soda kwa kuanza kukata kipande cha limao na kikamulie kwenye bakuli kisha weka unga kiasi wa Baking soda changanya mpaka upate uzito wa kukuwezesha wewe kutumia kusugulia kucha zako.

Chukua mswaki chovya mchanganyiko kisha sugua kucha zako.

Ukimaliza kusafisha kucha zako kwa kutumia maji ya limao, dawa ya mswaki na baking soda, unaweza kutumia maji ya mshumaa ili kusaidia kucha kuwa ngumu.

Unatakiwa kudondoshea matone ya mshumaa katika kucha na kuacha yale matone kwa muda wa dakika tatu kisha toa kwa uangalifu fanya hilo zoezi mara kwa mara ili kucha ziwe ngumu.

Unatakiwa kuwa makini usiunguze kwa sababu mshumaa unaunguza.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kababu za nyama na mayai

KABABU za mayai, ni chakula kitamu ambacho kinaweza kuliwa muda wowote, iwe mchana,asubuhi au jioni.

Chakula hiki kinapendeza kikasindikizwa na vinywaji baridi, kama juisi, soda au maji.

**Mahitaji**

Mahitaji ya kutengeneza kababu ni mayai saba, chenga za mkate, nyama ya kusaga robo kilo, tangawizi nusu kijiko, kitunguu saumu nusu kijiko, mafuta ya kupikia nusu lita, mkate, chumvi kiasi na pilipili manga kiasi.



**Jinsi ya kupika kababu za mayai**

Osha mayai manne na kuyachemsha hadi yaive vizuri.

Changanya nyama, chumvi , tangawizi, kitunguu saumu na pilipili manga, chemsha hadi ikauke.



Loweka mkate ndani ya maji hadi uwe laini, kamua mkate changanya na nyama.

Vunja mayai mawili, changanya vyema na nyama weka pembeni na menya mayai yaliyochemshwa.

Yeyusha unga wa ngano mayai ili yakauke, kila yai lilochemshwa lizungushie nyama sehemu zoote vizuri.

Piga yai, chukua madonge yenye nyama ndani na uyachovye kwenye yai na kisha viringisha kwenye chenga za mkate, kisha tia kwenye mafuta yanayochemka jikoni.

Zikishaiva na kubadilika rangi kuwa ya hudhurungi zitoe weka kwenye chujio zijichuje mafuta kwanza.

Utaendelea kupika zote hadi zimalizike na uweke kwenye sahani safi tayari kwa ajili ya kuliwa na kinywaji ulichoandaa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Sababu zinazochangia nyumba kuvuja

KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kuimiliki.

Lakini inapokuwa kinyume cha matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Andrew Kitale, anazungumzia sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya kukamilika ujenzi.

Anasema ziko sababu mbalimbali zinazochangia nyumba nyingi kuvuja ambazo watu wanapaswa kuzifahamu na kuchukua hatua wanapojenga nyumba ili kuzuia athari kutokea baadaye.

Kitale anaeleza kwamba miongoni mwa sababu kuu zinazochangia tatizo hilo ni pamoja na matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanaokoa pesa.

Sababu nyingine, baadhi ya vifaa vinavyovaliwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa si rafiki kwa paa, hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadae hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo hasa kama halikuezekwa kwa utaalam mzuri, hivyo kuvuja.



Sababu nyingine anasema ni muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.

Nyingine anasema ni ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka na kwamba kasoro kama hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalamu unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea katika matabaka matatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Anashauri kwamba njia nyingine ya kuepuka paa lako lisivuje ni kuwa makini kuchagua wataalam wa kukuezekea, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uezekaji na kukagua paa la nyumba yako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka na kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo kwa namna moja ama nyingine hutengeneza nyufa hususani vyuma na vitu vizito.

## Jinsi ya kutunza friji nyumbani



UTUNZAJI wa mashine za kupoozea na kugandisha vyakula yaani friji umekuwa changamoto kubwa kwa baadhi ya watu.

Idadi kubwa hutumia mashine hizi kwa ajili ya kutunza chakula, pia kupoozea vinywaji, lakini hawajui njia sahihi ya kuhakikisha vyombo hivyo vinadumu kwa muda mrefu.

Hizi ni baadhi ya njia za utunzaji ambazo zitakufanya vifaa vyako viendelee kudumu.

**1.** Safisha pembe za mlango wa friji au jokofu kwa kutumia maji ili kuondoa taka zilizoganda.


**2.** Punguza barafu iliyoganda katika kuta za friji kwani hizi husababisha kutumia umeme zaidi.

Unaweza kuzima hadi barafu iyeyuke, au futa kwa maji ya moto.

**3.** Hakikisha unapanga vitu visivyo na uzito mkubwa katika vyumba vya friji au jokofu.

**4.** Tumia upepo wa vaccum cleaner ili kupuliza vumbi angalau mara mbili kwa mwaka, kifaa hiki hupatikana kwa mafundi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
ACHA DATA 'ON' SIONDOKI
SIRI KALI
LONGO LONGO
'GHOSH!'
DUH! KUMBE WAPIGA KURA KILA 'ENGO' WANANI-MULIKA?
HADI "CHIMBO" NAKUMBUSHWA AHADI!
GESTI
NDANI YA KIBASI
NYIE WATOTO WENU MMEWAENDEKEZA ALAFU MNAKUJA KUTU-PIGIA KELELE HUMU!
HA HA HA HAA!
UKIMPIGA UONEVU ALICHOKIFANYA YEYE KWENDA NA WAKATI HA HA HAA!
ETI TOTO LINALIA LINAGALAGALA HALITAKI BUKU KISA MAFUTA YAMEPANDA NA SHULE IPO JIRANI!
NAPIGA NALALA HUMO HUMO!
ANGOJE AJITEGEMEE NDIO AENDE NA HUO WAKATI, LAKINI SIO MFUKONI MWANGU "ASITHUBUTU!"
UNABAHATI SIJAKUSWEKA SERO UKAKAE UKAVUTE HARUFU MBAYA
NIKILIEGEMEA LILE NDOO LA 'NNYA' KULE SERO HUWA NAPATA USINGIZI FASTA!
HIVI NITATOBOA KWELI?
FUNDI
"SPESHALISTI WA KUPINDA VIJORA NA MADELA"
MIMI MWENYEWE FUNDI LAKINI "ZIPU YANGU MBOVU!"
KAMA UMETUPANDISHIA KODI KWA MADAI MAFUTA YAMEPANDA, IPO SIKU UTATU-AMBIA TUSHUKE UBADILI MATAIRI YA NYUMBA
TENA WEWE WENZAKO WANA-KULALAMIKIA KILA SIKU UNAKULA CHIPSI MBELE YA WAKE ZAO!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UNALALAMA HUNA KAZI' WAKATI KAZI YAKO KUSENGENYA

HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yakiri hali bado tete Mariupol, Uingereza yazidi kumbana Rais Putin



Mwanamke akiwa hospitali na watoto wake wanaokabiliwa na utapiamlo uliosababishwa na ukosefu wa chakula baada ya janga la njaa kuikumba sehemu kubwa ya Kaskazini mwa Kenya na nchi jirani za Somalia na Ethiopia. **PICHA: BBC**

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amethibitisha kuwepo kwa ugumu wa mazungumzo ya namna ya kuwaondoa askari waliojeruhiwa katika eneo la Mariupol ambalo limezingirwa na kushambuliwa na vikosi vya Russia.

Akizungumza usiku wa kuamkia jana kuhusu hali ilivyo Azovstal, alieleza kuwa askari waliosalia wa Ukraine wanaopambana kulinda mji huo na ambao wengi wao wamejeruhiwa wanahitaji kuondolewa kwa ajili ya matibabu.

Mji wa Mariupol ulioko Kusini mwa Ukraine, ni muhimu kwa Russia kimkakati na imesababisha kuelekeza nguvu zao na kuushambulia ili kuuteka.

Zelensky alikiri mazungumzo ya namna ya kuwaondoa ni magumu na si rahisi.

"Majadiliano tata yanaendelea katika hatua nyinginre yenye lengo la kuwaondoa waliojeruhiwa vibaya," alisema.

"Tunafanya kila liwezekanalo kuwaondoa wote, kila askari wetu mlinzi," aliongeza.

Alisistiza kwamba wamekuwa wakitumia wapatanishi wenye ushawishi katika mazungumzo hayo, lakini hakutoa maelezo zaidi.

**VITA VITAMALIZIKA MWISHONI MWA MWAKA**

Mkuu wa kitengo cha kijasusi cha kijeshi cha Ukraine amesema vita kati ya nchi yake na Russia itafikia hatua ya mabadiliko katikati ya mwezi wa Agosti na huenda vikamalizika mwishoni mwa mwaka huu.

Katika mahojiano na Sky News, Meja Jenerali Kyrylo Budanov alisema kwamba kilele cha mapambano kitakuwa katika wiki ya pili ya mwezi Agosti na mashambulizi mengi ya kivita huenda yakafikia kikomo mwishoni mwa mwaka huu.

"Kutokana na hayo, tutaongeza upya nguvu ya Ukraine katika maeneo yetu yote ambayo tumepoteza ikiwa ni pamoja na Donbas na Crimea." Alisema .

Aliongeza kwamba Russia ikishindwa katika vita hivyo itasababisha kupinduliwa kwa Rais wa Russia Vladimir Putin, mapinduzi ambayo alidai kuwa tayari yanaendelea.

Alidai kuwa Rais Putin alikuwa katika hali mbaya sana kisaikolojia na kimwili na ni mgonjwa sana.

Katika hatua nyingine ripoti kutoka Ukraine zinasema Russia imelazimika kuondoa vikosi vyake kutoka Kharkiv, ikiwa ni dalili ya Ukraine kushinda vita katika mji huo.

**UINGEREZA YAWAWEKEA VIKWAZO 'WAPENZI' WA PUTIN**

Uingereza imemuwekea vikwazo mke wa zamani wa Rais wa Russia Vladimir Putin, na anayedaiwa kuwa mpenzi wake wa sasa kutokana na uvamizi wa Ukraine.

Lyudmila Ocheretnaya, ambaye alikuwa mke wa kiongozi huyo hadi 2014, na mwanariadha wa zamani wa Olimpiki Alina Kabaeva, wanakabiliwa na vikwazo vya kusafiri Uingereza na kuzuiwa kwa mali zao.

Uingereza sasa imewawekea zaidi ya watu 1,000 kwenye orodha yake ya vikwazo .

Waziri wa Mambo ya Nje, Liz Truss alisema Uingereza ilikuwa ikifichua na kulenga mtandao mbovu unaoendeleza maisha ya anasa ya Putin na itaendelea kuweka vikwazo kwa wale wote wanaosaidia na kuunga mkono uchokozi wa Putin hadi hapo Ukraine itakaposhinda.

Truss alisema vikwazo dhidi ya Russia vinapaswa kuondolewa tu wakati wanajeshi wake wote watakapoondoka Ukraine.

Tangu aachane na Putin, Lyudmila Ocheretnaya amefaidika kutokana na mahusiano ya kibiashara ya upendeleo na mashirika yanayomilikiwa na serikali na kuonyesha utajiri mkubwa ambao haujaelezewa, Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, Jumuiya ya Madola na Maendeleo (FCDO) ilisema.

Ilisema taarifa hiyo kuwa Kabaeva ni mbunge wa zamani wa Russia na mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi ya National Media Group, ambayo inaripotiwa kuwa kampuni kubwa ya kibinafsi ya vyombo vya habari nchini Russia.

## Watu milioni 20 wakabiliwa na njaa – UN

**NAIROBI,** KENYA

SHIRIKA la Chakula la Umoja wa Mataifa, limesema watu milioni 20 Afrika Mashariki wako katika hatari ya kukumbwa na janga la njaa.

Ilisema Ethiopia tayari inapambana na ukame mbaya zaidi kuwahi kutokea takriban nusu karne na Somalia asilimia 40 ya watu wako katika hatari ya kukosa kabisa chakula.

Katika maeneo mengi ardhi ni kavu, vumbi na isiyostawisha mazao. Mifugo iliyobaki hula majani yaliyonyauka, huku idadi kubwa ya watu wanakula chochote wanachoweza kupata.

Jacinta Atabo Lomaluk ambaye anaishi katika kijiji cha Lomoputh, alisema yeye na watoto wake watano wanakabiliwa na utapiamlo tangu Septemba mwaka jana.

Katika kijiji chenye watu wachache huko Turkana, Kaskazini mwa Kenya, wanakijiji wanaomba mvua, lakini hawawezi kujua lini itanyesha.

Msimu wa nne sasa mvua hazijanyesha na kusababisha uwepo wa ukame mbaya zaidi kuwahi kutokea katika miongo kadhaa.

"Hali inazidi kuwa mbaya kuliko ilivyowahi kuwa, ndiyo maana unaweza kuona dalili za njaa hapa." Alisema mwanakijiji mmoja Lomaluk.

"Natamani kungekuwa na usaidizi wa haraka kuwaokoa wanaokabiliwa na njaa, haswa watoto ambao wako hatarini," alisisitiza.

Lomaluk ni mmoja tu wa mamilioni wanaoathirika na athari ya ukosefu wa mvua. Familia zimekata tamaa ya kupata chakula na maji. Mamilioni ya watoto wana utapiamlo. Mifugo ambayo familia za wafugaji wanaitegemea kwa chakula na kuendesha maisha yao imekufa. Ukame unaenea zaidi katika kijiji hiki kidogo cha Kenya.

MAKALA

# NGO KWA MAENDELEO ENDELEVU



Na Magabilo Masambu - 0689157789

SEPTEMBA 2021, Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa agizo jijini Dodoma kuhusu kuandaa mkakati kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) nchini kupunguza utegemezi katika utekelezaji wa majukumu yao. Agizo hilo limekwishaanza kutekelezwa maeneo mbalimbali nchini na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inasimamia ukusanyaji wa maoni ya kuandaa mkakati utakaozifanya zijitegemee badala ya kuendeshwa kwa fedha za misaada na michango ya watu mbalimbali.

Kwa Kanda ya Kaskazini, kwa maana ya mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara, pia tulipata fursa hiyo Mei 12, mwaka huu. Mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis. Naibu Waziri alisema mpaka sasa kamati imekamilisha andiko la majadiliano, nyenzo za ukusanyaji wa taarifa na maoni kutoka kwa wadau mbalimbali pamoja na ukusanyaji wa taarifa na maoni kutoka kwa wadau, kazi ambayo inaendelea katika kanda zingine.

Nipongeze uamuzi huu wa serikali wa kuwashirikisha wadau katika mchakato wa kutoa maoni, jambo ambalo litawapa nafasi ya kupendekeza njia ambazo hazitakuwa vikwazo katika uendeshaji wa mashirika hayo. Ni wazo jema kama serikali imetambua kwamba mashirika haya yana mchango mkubwa kwa ustawi wa taifa katika kuwawezesha wananchi kujipatia fursa mbalimbali katika maeneo tofauti.

Ni ukweli kwamba, NGO zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi tangu uhuru. Tukizungumza katika elimu, afya na kilimo, zimekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kijamii. Tunao ushuhuda wa shule zetu ambazo zilikuwa chini ya mashirika hayo na baadaye serikali ikazichukua, Watanzania bila kujali dini ama rangi zao wakapata elimu, tunazo hospitali nyingi tu zilizoko chini ya mashirika na zinaendeshwa vema.

Upande wa ajira, lazima tukubali kwamba kuna ongezeko kubwa la Watanzania ambao wanahitimu masomo yao katika ngazi mbalimbali za elimu na ajira imekuwa changamoto. Kumbe haya mashirika yakisimama vizuri yakaweza kujiendesha yataendelea kuajiri watanzania wengi zaidi na kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana wengi.

Kutokana na ukweli huo, ndiyo maana serikali imeona umuhimu huo pia. Kuna wakati fulani miaka kadhaa iliyopita, tuliona mtazamo wa baadhi ya viongozi ndani ya serikali, wakijaribu kuuaminisha umma kwamba mashirika haya ni mabaya na kama tungaliendelea hivyo kwa kipindi cha miaka kadhaa, bila kubadili mtazamo huo, basi karibu yote yangekufa na kuua ajira za watu wengi.

Ninakubali kwamba katika msafara wa mamba na kenge wamo. Inawezekana yako mashirika ambayo yanaweza kutumiwa vibaya, lakini hayawezi kuwa yote. Kwa mantiki hiyo, wizara husika na serikali kwa ujumla kama mlezi ni lazima kuendelea kutazama nyendo za kila shirika kuona kama hao kenge wapo katikati ya mamba.

Mtazamo huu mpya wa sasa unaanza kuonyesha matumaini makubwa ya kuyafanya mashirika kufufuka tena. Kikubwa, pamoja na maoni yanayoendelea kukusanywa, ni muhimu mkakati usiishie kwenye maoni pekee bali pia kutazama sheria mpya kadhaa zilizopitishwa wakati fulani hapa kwa sababu pengine jambo hili la kisheria linaweza kuwa gumu kueleweka kwa watoa maoni. Kuna umuhimu mkubwa baada ya maoni, sheria zifumuliwe upya na kama zilikuwa na vikwazo ziondolewe. Huwezi kuzungumzia kujiendesha kwa mashirika hayo kama hayataruhusiwa kuanzisha miradi ya kujiingizia kipato au kama yanaruhusiwa kumekuwa na urasimu mkubwa katika kutoa vibali vya kufanya hivyo. Mambo kama hayo yanafanya mashirika haya yategemee misaada kutoka nje jambo ambalo linahatarisha usalama wa nchi. Ninasema hivyo kwa sababu misaada hiyo wanayopewa inaweza kuwa na masharti, ndiyo maana baadhi ya mashirika wakati fulani yalionekana kama yanatumika.

Ni muhimu sheria ziruhusu uanzishwaji wa miradi mbalimbali ya kujiingizia kipato katika mashirika hayo. Suala la msingi ni kuhakikisha mapato hayaingii mifukoni mwa watu binafsi bali yanatumika kutoa ajira na huduma za kijamii kwa mujibu wa malengo ya mashirika. Mfano shirika linalohusika pengine na kutunza watoto yatima, likianzisha kilimo cha mahindi likapata chakula na kuuza kwa ajili ya matumizi ya watoto kutakuwa na shida gani?

Ushauri wangu, mashirika yatumie nafasi hii kurekebisha mambo ambayo yamekuwa kero na kizuizi cha kufanya yasijitegemee miaka nenda rudi. Yanafanya kazi nzuri sana katika taifa hili lakini yale machache yanayopata fedha kutoka nje zenye masharti ambayo yanawahitaji kuivua nguo nchi, hakuna sababu ya kufanya hivyo.

Watanzania tumebarikiwa nchi nzuri sana. Tunahitaji kuilinda na kuithamini kwa wivu wa hali ya juu, serikali imeonyesha nia njema ya kutaka kushirikiana ndiyo maana leo mnakutana na wizara husika moja kwa moja ili kuhakikisha mnasimama bila misaada.

Nina imani na serikali kwamba maoni yote yanayochukuliwa yatafanyiwa kazi na hayatatumiwa kupata uhalali wa kupitisha sheria ambazo zitakuwa mwiba kwa mashirika na kwamba malalamiko yakitokea baadaye basi utetezi uwe kwamba "Nyinyi ndio mliotoa maoni haya". Naamini kwamba yale yote yanayolalamikiwa kwenye maoni yatachukuliwa kwa uzito na kubadilishwa kwa kuzingatia maslahi ya taifa kwa ajili ya ulinzi wa utamaduni, mila na desturi zetu kama taifa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Napenda Nipate Lau Nafasi', ni nyimbo zilizoigwa toka Congo DR



Na Adam

KWENYE miaka ya 1960, bendi nyingi za Tanzania zilikuwa na tabia ya kuiga nyimbo kutoka Zaire ambayo sasa inajulikana kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kuiga nyimbo hakujaanza leo, ila kwa sasa ni mbaya sana kwa sababu kuna teknolojia ambazo zinaweza kumbaini mtu aliyeiga wimbo hata akiutoa leo leo na vipo vyombo ambavyo vinasimamia haki hiyo kwa kumtoza faini aliyeiga.

Zamani hata mwenzako akiiga, utamfanya nini na utampeleka wapi? Wakongo walikuja nchini na kukuta nyimbo zao zimeigwa na kurekodiwa, walishangaa lakini hawakuwa na la kufanya.

Dunia kwa sasa ni kama kijiji, hivyo wanaoiga nyimbo za wenzao, tunaona ni nini kinachowatokea. Ni kwamba vipo vyombo vinavyolinda haki ya wanamuziki dunia nzima, hivyo ni lazima alipe tu. Ni kama mwanamuziki Michael Jackson alipotoa kibao cha 'Wanna Be Startin Somethin', ambacho kilikuwa na kipande cha wimbo wa mwanamuziki Manu Dibango wa Cameroon kwenye wimbo wake wa 'Soul Makosa'. Kilichotokea ni kwamba Manu Dibango alishtaki na Michael alimlipa pesa nyingi zilizomtajirisha mwanamuziki huyo hadi alipofariki dunia mwaka 2020. Michael yeye alifariki dunia mwaka 2009. Huu ni mfano unaoonyesha jinsi sheria ya hakimiliki inavyofanya kazi duniani, hasa kwenye miaka ambayo teknolojia imetamalaki.

Nikisema hivi sisemi kuwa bendi hairuhusiwi kupiga 'laivu' nyimbo za bendi zingine, hapana. Dunia nzima bendi haiwezi kupiga nyimbo zake peke yake kwenye steji hata huko Congo DR, ambako kuna wanamuziki mahiri. Ambacho hakiruhusiwi ni kurekodi wimbo wa bendi, kundi au mwanamuziki mwingine, ila kupiga laivu hiyo haikatazwi popote pale.

Tunarudi kule miaka ya 1960, bendi za Zaire zilikuwa moto na zilitoa vibao mbalimbali ambavyo vilitamba Afrika nzima, ikiwemo nchini Tanzania. Kutokana na nyimbo hizo kupendwa sana, baadhi ya bendi nchini zikaanza kuiona fursa ya kuziiga.

Walikuwa wakizipiga hivyo hivyo zilivyo na kwa umahiri mkubwa. Walichofanya ni kubadili maneno na maudhui. Nyimbo za wanamuziki wa Zaire ziliimbwa kwa lugha ya Kilingala, lakini huku sasa zikabadilishwa na kuimbwa kwa Kiswahili. Na mara nyingi, maana inakuwa ni nyingine kabisa. Walichoimba Wazaire, sicho kilichorudiwa na Watanzania, ila mirindimo ilikuwa inafanana vile vile, kiasi kwamba huwezi hata kujua nani alimuiga mwenzake.

Ukweli unabaki pale pale kuwa Watanzania kwa nafasi kubwa waliiga nyimbo nyingi kutoka Zaire ambayo kwa sasa ni Congo DR.

Hata hivyo zipo baadhi ya nyimbo ambazo pia Wacongomani waliiga kutoka Tanzania, hii itakuwa mada ya wiki ijayo, lakini leo tuendelee na hii. Ilifika wakati sasa serikali ya Tanzania kupitia wizara husika ya utamaduni, ilibidi ipige marufuku bendi za Tanzania kuiga na kuzibadilisha nyimbo za Kizaire na kuziimba Kiswahili. Wakaambiwa watunge za kwao, kuanzia maneno mpaka mirindimo. Huo sasa ukawa ndiyo mwisho wa bendi za Kibongo kuwa na tabia hiyo.

Hebu tuziangalie nyimbo maarufu ambazo zilirudiwa na bendi za Tanzania.

Tunaanza na wimbo maarufu wa Kilwa Jazz Band, chini ya kiongozi wake Ahmed Kipande, uitwao 'Napenda Nipate Lau Nafasi'. Huu hadi leo hii vijana wa kizazi kipya wanaufahamu na kuupenda. Ni wimbo wa katikati ya miaka ya 1960. "Napenda nipate lau nafasi, nipate kusema nawe kidogo aah mama, mwenzio naumia.

Hakika la kufanya bado sijaliona, nimeona bora leo nikuimbie,

huenda roho yangu ikadunda, ukaja siku ukajanipoza moyo oh mama, rohoni naumia.

Hakika kuja kwako ewe wangu mpenzi, ni kama mganga utayenitibu, katika maradhi yanayonisibu, hakuna mwingine ila ni wewe mpenzi uje hima, roho naumia."

Asili ya wimbo huu ni 'Mokolo Nakokufa' uliopigwa na African Fiesta, ukiimbwa na Tabu Ley Rochereau, mwanzoni mwa miaka ya 1960. Ukizisikiliza nyimbo hizo mbili zinafanana sana, utofauti uko kwenye maneno tu. Huku Kiswahili na huku Kilingala. Maudhui nayo ni tofauti pia.

Kilwa Jazz waliuiga wimbo huu, wao wanaufanya wa mapenzi, lakini Tabu Ley yeye alikuwa akiimba kuwa siku akifa, hajui atakufa kifo cha aina gani? Ni cha maji, ajali ya gari, au kuumwa? Siku akifa masikini ataacha watoto wanalia. Siku atakapokufa tajiri, ataacha magari aliyonunua na nyumba za kifahari. Siku atakapokufa msichana mrembo ataacha wapenzi wake, vipodozi na nguo nzuri za gharama, na siku akifa mlevi, ataacha makopo ya pombe.

Kilwa Jazz hao hao, ambao walikuwa mahiri sana kuiga nyimbo za Kikongo waliiga wimbo mwingine wa TP OK Jazz, chini ya Franco Luambi Luanzo Makiadi uitwao 'Course au Pouvoir'.

Hiyo ni mwishoni mwa miaka ya 1960. Wao wakauita 'Nachekacheka Kilwa Leo'. Nao haukutofautiana sana na ule wa wenyewe. Mpaka gita la solo linapokuwa linashindana na saxophone, kiasi cha kulia kama jogoo 'kokorikooo' na wanamuziki wanashangilia eee, vipande vyote vilikuwa kwenye nyimbo zote mbili. Dar Jazz nao waliiga wimbo wa TP OK Jazz ya Franco uitwao 'Quatre Boutons', wao wakauita 'Mtoto Aacha Kupiga Mayowe' wanauimba "Mtoto acha kupiga mayowe, waachie watu waone wenyewe."

Wimbo wa 'Mindondo Ya Kosuana Na Mobali' wa Franco, pia uliigwa na NUTA Jazz, wao wakauimba kusifia 'Azimio la Arusha' la mwaka 1967. "Sisi wote ooo twakubali oo, Azimio ooo la Arusha ooo".

Ndala Kasheba, akiwa na Orchestra Safari Sound mwanzoni mwa miaka ya 1980, alirekodi wimbo mmoja ulioitwa "Uliomba Tucheze'. Huu waliuiga kutoka pia TP OK Jazz, utunzi wake Ntesa Dalientst uitwao 'Bina Ngai na Respect', yaani cheza na mimi kwa nidhamu.

Maneno ni yaleyale, nadhani hawa hawakubadilisha maneno kwa sababu wao wenyewe walikuwa na asili ya Congo, walichofanya ni kutafsiri tu. "Mara ya kwanza uliniomba tucheze, muziki wa kwetu siwezi kukataa, mara ya pili umerudia tena. Siyo kwa kucheza ila kunifinya jicho, uliza kwanza kabla ya kufanya upuuzi wako bwana wee, nimeshaolewa, nimekuja kufurahisha mwili wangu bwana ee, mimi ni mke wa watu.

Na mume wangu yupo hapa hapa, ameniruhusu kucheza muziki wa kwetu, tafadhali bwana. Duku duku ni wasiwasi wao, muziki wetu unatia fora."

Hizi ni baadhi tu ya nyimbo nyingi ambazo bendi za Tanzania ziliiga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kutamba sana nchini, kabla ya serikali kupiga marufuku. Wiki ijayo tutaziangalia pia za wanamuziki wa huko, pamoja na umahiri wao wote, waliiga kutoka kwa Watanzania.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18, alikimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabishara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki dunia kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je, ni wafanyabishara wenzake Chilambo ndio waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya Siri-28

Na Adam Fungamwangwo
(0716 350534)

ALIPOWASHA TV tu, kilichokuwa kikionekana ni kuanza kwa taarifa ya habari ya ITV, saa mbili usiku. Na habari iliyokuwa kubwa siku hiyo ni hukumu ya mtuhumiwa wa mauaji, Tina Kauzeni.

"Mahakama ya Rufaa imemwachia huru Tina Kauzeni mwenye umri wa miaka 18 aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji ya bosi wake miezi sita iliyopita.

"Awali, Mahakama Kuu ilimhukumu msichana huyo kunyongwa hadi kufa kutokana na kupatikana na hatia ya kumuua Hafidh Chilambo kwa kumwekea kwenye chakula aina mbili za dawa ambazo zikichanganywa zinageuka kuwa sumu.

"Hata hivyo. kesi hiyo ilikatiwa rufani kweye Makakama ya Rufani na kusimamiwa na Wakili Florence Tinga hadi baadaye mtuhumiwa kuwa huru.


Taarifa zinasema kuwa mpelelezi maarufu nchini, Eddy Kamal, ndiye aliyefanya kazi hiyo ya kukusanya ushahidi na vielelezo visivyo na shaka ambavyo vimetumika kumwondoa hatiani mtuhumiwa.

"Wakati huo huo, Jeshi la Polisi limewakamata mke wa marehemu Chilambo, Hellen Kisa na mtu mmoja anayefahamika kwa jina la Abdallah Mtola kutokana na kushukiwa kuhusika na mauaji hayo.

"Katika ushahidi uliomwondoa hatiani Tina, ambaye alikuwa dada wa kazi kwenye nyumba ya marehemu Chilambo, ni kwamba Hellen na Mtola wanaonekana kuhusika na mauaji hayo. Jeshi la Polisi limesema kuwa litautumia ushahidi huo huo wa mpelelezi Eddy, kwenye kesi ya mauaji itakayofunguliwa hivi karibuni.

"Imesema kuwa inafungua kesi kwa watu hao wawili ya kula njama kumuua Chilambo kwa kumwekea sumu au dawa zilizogeuka kuwa sumu ili kumuua.

Na sababu kubwa imeelezwa ni kwamba watuhumiwa hao wawili ni wapenzi, hivyo walikula njama hiyo ili kwanza Hellen




**Tangu mdogo ilikuwa ndiyo kazi yake. Anakumbuka kila Jumamosi na Jumapili, kazi ilikuwa ndiyo hiyo. Awali ilikuwa ngumu, lakini kadri muda ulivyozidi alianza si tu kuizoea, bali kuipenda pia. Kwake ilianza kuwa kama mchezo wa kitoto.**

arithi mali za marehemu mumewe, halafu kizuizi kiondoke, waoane. Walikuwa na ajenda ya siri.

Limesema kuwa watuhumiwa hao walifanya hila ili ionekane mfanyakazi wa ndani Tina kuwa muuaji, ili kuficha wao kujulikana,"ilisomeka taarifa hiyo katika televisheni.

Eddy alikuwa amekaa subuleni, akiwa amevaa pensi, kifua wazi akisikiliza na kuifuatilia kwa makini taarifa hiyo ya habari.

Cha ajabu wakati ikitangazwa alionekana kama na yeye kushangaa kama mtu ambaye anayekisikia kisa hicho kwa mara ya kwanza.

Mwahija alitoka jikoni akiwa na kikombe cha chai, silesi mbili za mikate na mayai ya kukaanga. Akayaweka akampelekea Eddy.

"Mwanaume mwongo wewe." Sauti ya Mwahija ilipenya vizuri kwenye masikio ya Eddy wakati akipiga funda la kwanza la chai.

"Kwa nini?"

"Hivi uongo utakusaidia nini mwaya?" "Mbona sikuelewi Mwahija, nimekudangaya nini?"

"Kumbe Danny ndiyo Eddy Kamal?" Sasa Eddy alijua kwa nini Mwahija aliongea hivyo.

Hakushtuka. Alijua Mwahija atajua kuwa yeye ni nani. Lakini hakutaka yeye kumwambia. Alitaka ajue mwenyewe.

"Danny ni jina la utoto, Eddy ni jina la ubatizo." "Na wewe kuwa mjomba wa Tina nayo imekuwaje?"

"Sina la kujibu, yote unayajua. Kama umeshajua mimi ni nani, basi nadhani umeshajua kwa nini sikukwambia mimi ni nani na kwa nini nilikwambia ni mjomba wa Tina."

Ni kweli Mwahija alijua kuwa mpenzi aliye naye si Danny, bali ni mpelelezi maarufu nchini, Eddy Kamal, wakati kesi ya Tina ilipomalizika. Aliwasikia na kuona watu wengi wakimzungumzia mahakamani hapo na kunyoosha vidole kwake, wakimshangaa na kumpongeza. Ni wakati akiwa ametoka na kuongea na Tina, pamoja na watu wengine.

Alishangaa, lakini alipoanza kurudisha picha nyuma tangu mwanzo alipomwona kwa mara ya kwanza kwenye famasi anayofanyia kazi, hadi kazi alizokuwa akitumwa kutafuta majina na walipo wafanyakazi wa nyumba ya marehemu Chilambo, picha ikaanza kumjia kuwa ni kweli, mpenzi wake hakuwa mtu wa kawaida. Na hata siku ya kwanza alipofika kwenye famasi anayofanyia kazi Tegeta, alikuwa yupo kazini kupeleleza na kusaka ushahidi wa kesi ile.

"Si ungeniambia mapema kama ni wewe ili nitambe kuwa nina mpenzi mpelelezi? Nilianza kukusikia na kukusoma zamani wakati nipo shule ya sekondari."

"Si umeshanijua, haya tamba sasa." Mwahija aliishia kucheka.

Ghafla, Eddy alimshika mkono wa kushoto Mwahija. "Fumba macho?" Mwahija alishtuka. Lakini akafumba kidogo. Kuna kitu kilionekana kupenya kwenye kidole chake cha pili kutoka mwisho.

Akafumbua macho ghafla. Akapatwa na mshtuko mwingine. Safari hii ulikuwa wa furaha.

"Ha..., waooo." Alipiga kelele. Alimkumbatia kwa nguvu Eddy, nusura amwage na chai yenyewe. Kwa muda mrefu wakati amekaa pale alikuwa na pete mkononi. Alikuwa anataka Mwahija alete chai, ili amvalishe. Ilikuwa 'sapraizi' ya aina yake.

"Utanioa kweli mpenzi." Ni kama vile alipagawa.

"Nilikwambia na nilimwambia mama yako mdogo jambo hili. Nadhani mmesahau au hamkuamini."

"Kwa kweli mwenzangu siamini."

"Basi we endelea kutoamini."

"Nakupenda sana Eddy wangu."

"Nami pia nakupenda"

Wapenzi hao walibaki wamekumbatiana, huku kila mmoja akiwaza jinsi walivyokutanishwa kwa bahati tu kutokana na sakata la binti Tina Kauzeni.

**MWISHO**

**■ Sehemu hii ya mwisho ya hadithi imerudiwa kutokana na sababu za kiufundi. Hadithi mpya ya Mwisho wa mauaji iliyoanza Jumapili iliyopita, itaendelea Jumapili ijayo- MHARIRI.**



## UZUNGU UMEWAPONZA

# Watakiwa kujitathmini kwanza

LICHA ya wasanii kutoka lebo ya WCB, kulalamikia kitendo cha serikali kuubana wimbo wa 'Mtasubiri', wameshauriwa kuacha tabia ya uzungu mwingi katika kazi zao.

Baadhi ya watu wametoa maoni kufuatia Baraza la Sanaa Tanzania (Basata) na TCRA kuufungia wimbo huo kutokana na baadhi ya sehemu kutokwenda na maadili ya Kitanzania.

"Unajua WCB wanatakiwa kujitathmini badala ya kulalamika, nyimbo zao nyingi zina uzungu mwingi kiasi ambacho huwezi kutazama na familia yako. Wasilaumu tu wanatakiwa wajipange kuhakikisha kazi zao zinatazamwa na kila mtu," amesema Monica Mziwanda.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Basata Matiko Mniko, naye ametoa ushauri kwa kuwataka Diamond Platnumz na Zuchu kufanya marekebisho ya video yao ili kufunguliwa.

"Video yao itaruhusiwa na kuendelea kuruka hewani endapo wakifanya marekebisho," amesisitiza.

# Huyu ndiye Kendrick Lamar mpya

MWANAMUZIKI wa Marekani, Kendrick Lamar, ameonjesha ujio wa Albam yake mpya inayoitwa 'Mr. Morale & The Big Steppers' baada ya kukaa kimya kwa miaka mitano.

Lamar alitoa album yake ya mwisho ya 'Damn' na baada ya hapo hakuonekana jukwaani jambo ambalo liliwafanya mashabiki wake kumlalamikia.

Album hiyo ina jumla ya nyimbo 18 ambazo pia amefanya colabo na wasanii nyota kama Summer Walker, Ghostface Killah, Baby Keem, Kodak Black na Blxst.

Katika kava ya album anaonekana Kendrick Lamar akiwa amembeba binti yake wa miaka miwili, huku mchumba wake Whitney Alford naye anaonekana akiwa na mtoto wao mchanga aliyezaliwa hivi karibuni.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE NA MADRID

KLABU ya Real Madrid inajiamini kuliko wakati wowote" kwamba wanaweza kukamilisha usajili wa mshambuliaji wa Ufaransa na Paris St-Germain, Kylian Mbappe, lakini nyota huyo mwenye miaka 23 hajaamua kuhusu mustakabali wake. ***(Fabrizio Romano)***

### GRIEZMANN HATAKIWI BARCA

BARCELONA hawana mpango wa kumrejesha Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31 kama Atletico Madrid hawataamua kubaki nae ambako anacheza kwa mkopo. ***(Cuatro)***

### LEWANDOWSKI HAACHIWI

RASI wa Bayern Munich, Herbert Hainer amesema Robert Lewandowski ana mkataba na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga hadi Juni 2023. ***(Sport Buzzer)***

### PERISIC HUYO CHELSEA

CHELSEA imefikia makubaliano ya awali ya kumsajili winga wa Croatia, Ivan Perisic mwenye umri wa miaka 33 kutoka Inter Milan. ***(Mediaset, via Metro)***

### DE JONG HATAKI

KIUNGO wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, anajiandaa kukataa kuhamia Manchester United. ***(Star)***

### BELLINGHAM HAONDOKI

KIUNGO wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18 amezungumzia tetesi zinazomuhusisha kuhamia kati ya Manchester United au Liverpool kwa kuthibibitisha kwamba atabakia Borussia Dortmund msimu ujao. ***(Mirror)***

### ALLEN AGOMBEWA

KLABU ya Swansea City inakabiliana na ushindani kutoka klabu zilizopanda ligi kuu za Fulham na Bournemouth katika kumsajili kiungo wa Wales, Joe Allen mwenye umri wa miaka 32 kutoka Stoke City. ***(Wales Online)***

### LUKAKU HATAKI UPUUZI

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, amesema "hataruhusu mtu kuzungumza kwa niaba yake" baada ya wakala wake Federico Pastorello kuzungumza na gazeti moja la Italia kuhusu uwezekano wa kurejea Italia. ***(Star)***

### WAKALA WA DYBALA

WAKALA wa mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, ameelezwa yuko London kufuatilia ofa kutoka klabu za ligi kuu, ikiwemo Arsenal. ***(Calciomercato via Football Italia)***

### TARKOWSKI AWINDWA

KLABU ya West Ham iko tayari kujiondoa katika mbio za kumsajili beki wa kati wa Burnley, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU ASEMA HAONDOKI CHELSEA

**●●● Amjibu wakala wake baada ya kusema kwamba hana furaha Chelsea na yeye amesema hana...**

**LONDON,** England

ROMELU Lukaku anaonekana kumkasirikia wakala wake, Federico Pastorello baada ya kusema kuwa mshambuliaji huyo hana furaha Chelsea na anataka kurejea Inter Milan.

Lukaku ameanza kuwa kwenye ubora wake katika siku za hivi karibuni baada ya kurejea Chelsea kwa pauni milioni 97.5 kutoka Inter Milan, akifunga mabao mawili dhidi ya Wolves na kufunga katika mechi yake ya mwisho dhidi ya Leeds United.

Hilo linamfanya afikishe mabao nane kwa msimu huu kwenye Ligi Kuu ya England katika mechi 25 alizocheza.

**Kocha wake, Thomas Tuchel alishangaa baada ya Pastorello kufichua mipango ya mustakabali wa mshambuliaji huyo, akisema "ni dhahiri kwamba kulikuwa na tatizo".**

Pastorello alidokeza kuwa Lukaku anaweza kurejea Italia, kwa sababu hafurahii tena kucheza hapo Chelsea.

Katika mahojiano ya Pastorello na La Republica, alidokeza kuwa klabu ya zamani ya Inter au hata majirani zake AC Milan walikuwa wanamuwania Lukaku.

Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Sitawahi kuruhusu mtu anisemee. Nilifunga mdomo wangu na kulenga kusaidia timu na kumaliza msimu kwa njia bora iwezekanavyo.

"Kwa hiyo kama mtu huko nje (anajaribu) kusema jambo fulani kuhusu mimi na klabu... si kwa jina langu"

Sio mara ya kwanza kwa mustakabali wa Lukaku ndani ya Chelsea kutiliwa shaka baada ya nyota huyo kunukuliwa na Sky Sport Italia akisema "kutofurahishwa" na nafasi yake katika mipango ya kikosi cha kwanza cha Tuchel Desemba.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
WEST HAM
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 6.46
X | 4.62
2 | 1.41

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GERRARD AMFAGILIA COUTINHO



**LONDON,** England

PHILIPPE Coutinho atapanda "kiwango kingine" baada ya kukubali uhamisho wa kudumu kutoka Barcelona na kutua Aston Villa, kwa mujibu wa kocha, Steven Gerrard.

Villa ilitangaza Alhamisi kwamba Coutinho atakamilisha uhamisho wa pauni milioni 17 mwishoni mwa msimu huu, baada ya kuwa kwenye kiwango bora akicheza kwa mkopo kwa nusu msimu katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ametengeneza nafasi nyingi zaidi kati ya wachezaji wa Villa (24) tangu kufunga na kusaidia mechi yake ya kwanza dhidi ya Manchester United, Januari 15 mwaka huu. Coutinho pia ametengeneza nafasi nyingi zaidi katika kipindi hicho (tano) kuambatana na mabao yake manne na asisti tatu.

Kocha wa Villa Gerrard alielezea furaha yake ya kupata saini ya Coutinho na akapendekeza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 atakua na kiwango bora zaidi hapo Villa Park.

Alipoulizwa kuhusu Coutinho, Gerrard alitania kwa kuwaambia waandishi wa habari: "Pengine mkali wangu."

Aliongeza: "Nilikuwa najua kidogo kabla ya kutangazwa, na nadhani ni nzuri kwa kila mtu aliyeunganishwa na klabu.

"Umeona majibu kutoka kwa mashabiki, ni chanya sana, wamemuona katika kipindi cha miezi mitano au sita iliyopita akicheza vizuri sana.



## *Lampard hana hofu kwa Calvert-Lewin*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Everton, Frank Lampard "hana wasiwasi hata kidogo" kuhusu Dominic Calvert-Lewin, ambaye amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka hapo Goodison Park.


Calvert-Lewin alikuwa bora kwa Everton msimu uliopita, akifunga mabao 16 ya Ligi Kuu England, lakini msimu huu amekumbwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amefunga mabao matatu pekee, huku yote yakitoka katika mechi tatu za ufunguzi wa msimu huu, huku mawili kati yao yakitokana na mikwaju ya penalti.

Rafael Benitez alitaka kuendeleza mtindo uliowekwa na Carlo Ancelotti na kumfanya Calvert-Lewin kuwa moyo wa safu ya ushambuliaji ya Everton, lakini baada ya kuvunjika kidole cha mguu Agosti, fowadi huyo alipata jeraha baya jingine ambalo lilimfanya kukosa kucheza kwa zaidi ya miezi minne.

Calvert-Lewin alirejea mwanzoni mwa 2022, kuelekea mwisho wa kipindi kibaya cha Benitez, lakini ameshindwa kuwa kwenye mipango ya Lampard huku Everton wakipigania kubakia Ligi Kuu England.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA



# MORRISON AWEKWA MTU KATI

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kutangaza kumpa mapumziko hadi mwishoni mwa msimu, klabu ya Simba imesema kuwa suala la kurejea kwenye klabu hiyo au kutorejea lipo mikononi mwake mwenyewe.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema Morrison anaweza kuamua kwenda kwingine kama akiamua, kwani msimu ukimalizika na mkataba baina yake utakuwa umemalizika.**

"Sisi Simba mpaka sasa hatujaamua mchezaji gani aondoke na nani asalie, tunasubiri mwisho wa msimu. Ligi ikiisha, ripoti ya mwalimu ndiyo itakayoamua nani inamhitaji na nani haimhitaji, kwa hiyo huwezi kumwambia akae hadi asubiri benchi la ufundi, lakini yeye mwenyewe ndiyo anaweza kuamua hivyo na si klabu imwambie," alisema Ahmed.

Kupewa mapumziko kwa mchezaji huyo hadi mwishoni mwa msimu kumezua mjadala mkubwa, huku baadhi ya mashabiki wa soka, wakiona ni njia ambayo wameitumia Simba kuachana na mchezaji huyo mtukutu.

Akitoa ufafanuzi wa hilo, Ahmed alisema taarifa yao iliandikwa kumtakia kila la kheri kwa sababu anakwenda kutatua matatizo yake, lakini pia kumtakia kila la kheri kwenye maisha yake ya kimpira kwa sababu ndiyo kazi yake, hivyo anaweza kuamua kwenda kwingine kama akitaka.

"Tumempa mapumziko kwa sababu yeye mwenyewe alitufuata, akasema ana mambo mengi binafsi yanamtatiza na angependa kupata muda wa kwenda kuyashughulikia, klabu kwa kujali maslahi ya mchezaji tukaona tumpe nafasi kwenda kuyakabili, unaweza kumng'ang'ania mtu halafu shida alizonazo zikasababisha asikupe kile unachohitaji kutoka kwake," alisema Ahmed.

Alisema hata Morrison mwenyewe aliandika kuwa anaomba matatizo yake yamalizike ili arejee, hivyo milango bado iko wazi. Hata hivyo kumekuwa na tetesi za kumhusisha kurejea kwenye klabu yake ya zamani ya Yanga.

Baadhi ya watu wa karibu na klabu hiyo kwa siku za karibuni wamekuwa wakiweka video zake fupi kwenye mitandao ya kijamii, za wakati huo akiichezea, miaka miwili iliyopita, wakichombeza na maneno yanayoashiria kuwa na ukaribu naye.



Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls wakiwa kwenye mazoezi katika Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha kujiandaa na mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Cameroon utakaopigwa Mei 19 mwaka huu. **PICHA: TFF**

# *Simba Queens yatwaa Ubingwa Bara*

Na Adam Fungamwango

TIMU ya soka ya wanawake ya Simba Queens, juzi ilifanikiwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, baada ya kuifunga Mlandizi Queens mabao 2-1 kwenye mechi iliyochezwa, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Hii inakuwa ni mara ya tatu mfululizo kwa timu hiyo kutwaa ubingwa. Simba Queens imefanikiwa kuwa bingwa, huku ikisalia na mechi mbili mkononi.

Ilihitaji pointi tatu tu iweze kutawazwa ubingwa kwani imefikisha pointi 57 ambazo haziweza kufikiwa na timu yoyote ile.

Yanga Princess ambayo iliibamiza Ilala Queens mabao 5-1 juzi kwenye Uwanja wa Karume, Dar es Salaam, hata kama ikishinda mechi zake mbili zilizobaki itafikisha pointi 56 tu, huku timu nyingine iliyokuwa tishio kwa mabingwa wao, Fountain Gate Princess ililazimishwa suluhu dhidi ya TSC Queens kwenye Uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza.

Ikihitaji pointi tatu, haikuwa kazi rahisi kwa Simba Queens ambao wachezaji wake walionekana kuwa na papara ya ubingwa, hivyo kukosa mabao mengi ya wazi.

Dakika ya 17, straika tegemeo wa timu hiyo kwa sasa baada ya kuondoka kwa Opah Clement, Mrundi Asha Djaffar alipachika bao ambalo lilidumu hadi dakika ya 38, pale Victtoria Moshi aliposawazisha bao hilo ambalo liliweka roho juu mashabiki wa Simba Queens.

Ilibidi wasubiri hadi dakika ya 56 kupata bao la pili lililofungwa na beki wa kulia wa timu hiyo, Sylvia Mwacha, alipopiga shuti lililombabatiza beki mmoja wa Mlandizi Queens na kutinga wavuni. Timu hiyo imetwaa ubingwa ikiwa ina pointi hizo 57 na mabao 90, ikifungwa mabao saba tu.

Kabla ya mechi mbili kumaliza msimu, imecheza mechi 20, ikishinda 19 na kupoteza mmoja, ikiwa haijatoka sare yoyote mpaka sasa.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 15/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4904 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.70 | 2.57 |
| 14:00 | 5217 | Tottenham vs Burnley | 1.32 | 5.14 | 7.70 |
| 15:30 | 1691 | PEC Zwolle vs PSV Eindhoven | 5.94 | 4.75 | 1.43 |
| 15:30 | 2887 | AZ Alkmaar vs Waalwick | 1.21 | 6.32 | 10.87 |
| 15:30 | 2976 | Vitesse Arnhem vs Ajax | 6.34 | 4.96 | 1.39 |
| 15:30 | 3293 | Heracles Almelo vs Sparta Rotterdam | 2.29 | 3.02 | 3.22 |
| 15:30 | 3330 | Feyenoord vs Twente | 1.47 | 4.56 | 5.56 |
| 15:30 | 4052 | NEC Nijmegen vs Fortuna Sittard | 2.17 | 3.52 | 2.98 |
| 15:30 | 4557 | Heerenveen vs GO Ahead Eagles | 1.86 | 3.61 | 3.76 |
| 16:00 | 1198 | Aston Villa vs Crystal Palace | 2.01 | 3.41 | 3.46 |
| 16:00 | 2275 | West Ham vs Manchester City | 6.46 | 4.62 | 1.41 |
| 16:00 | 2338 | Trabzonspor vs Altay | 1.37 | 4.97 | 6.95 |
| 16:00 | 2432 | Ostersunds vs IK Brage | 2.83 | 3.38 | 2.43 |
| 16:00 | 2496 | Napoli vs Genoa | 1.75 | 3.78 | 4.08 |
| 16:00 | 4097 | Watford vs Leicester | 3.31 | 3.51 | 2.03 |
| 16:00 | 4192 | Wolverhampton vs Norwich City | 1.43 | 4.35 | 6.73 |
| 16:00 | 4296 | Leeds vs Brighton | 2.58 | 3.37 | 2.53 |
| 16:00 | 5674 | Goeztepe vs Besiktas | 4.37 | 4.37 | 1.62 |
| 16:30 | 2429 | Spartak Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.56 | 3.76 | 1.88 |
| 18:30 | 1953 | Everton vs Brentford | 2.05 | 3.42 | 3.32 |
| 18:30 | 3547 | Degerfors vs Helsingborg | 2.36 | 3.22 | 2.73 |
| 18:30 | 4159 | IFK Goteborg vs Varbergs Bois | 1.74 | 3.36 | 4.38 |
| 18:30 | 5599 | Norrkoping vs GIF Sundsvall | 1.35 | 4.67 | 6.81 |
| 19:00 | 1023 | Alanyaspor vs Gaziantep BB | 1.60 | 4.06 | 4.95 |
| 19:00 | 1703 | Fenerbahce vs Fatih Karagumruk | 1.46 | 4.60 | 5.80 |
| 19:00 | 2819 | Aalborg vs Brondby | 2.04 | 3.48 | 3.38 |
| 19:00 | 2975 | Giresunspor vs Basaksehir | 3.88 | 3.38 | 1.92 |
| 19:00 | 3226 | IK Start vs Sogndal | 1.89 | 3.55 | 3.46 |
| 19:00 | 4233 | Stjordals-Blink vs Ranheim | 2.48 | 3.40 | 2.48 |
| 19:00 | 4707 | Kasimpasa vs Antalyaspor | 1.98 | 3.67 | 3.37 |
| 19:00 | 5257 | FC Krasnodar vs CSKA Moscow | 3.07 | 3.62 | 2.09 |
| 19:00 | 5695 | Konyaspor vs Hatayspor | 1.62 | 4.08 | 4.68 |
| 19:00 | 5741 | AC Milan vs Atalanta | 1.74 | 3.96 | 3.96 |
| 19:30 | 2281 | Asteras Tripolis vs Apollon Smyrnis | 1.47 | 4.07 | 6.75 |
| 19:30 | 2720 | Lamia vs Atromitos | 2.54 | 3.09 | 2.79 |
| 20:00 | 3227 | Famalicao vs Sporting Braga | 2.93 | 3.53 | 2.22 |
| 20:30 | 1668 | Levante vs Alaves | 2.95 | 3.50 | 2.24 |
| 20:30 | 1796 | Mallorca vs Rayo Vallecano | 1.59 | 3.71 | 5.81 |
| 20:30 | 1835 | Athletic Bilbao vs Osasuna | 1.54 | 4.01 | 5.81 |
| 20:30 | 2758 | Cadiz CF vs Real Madrid | 3.02 | 3.21 | 2.34 |
| 20:30 | 2821 | Getafe vs Barcelona | 3.43 | 3.20 | 2.15 |
| 20:30 | 2851 | Atletico Madrid vs Sevilla FC | 2.29 | 3.00 | 3.35 |
| 20:30 | 3733 | Villarreal vs Real Sociedad | 2.18 | 3.45 | 3.10 |
| 20:30 | 4065 | Betis vs Granada | 1.51 | 4.31 | 5.62 |
| 21:45 | 4535 | Cagliari vs Inter | 6.95 | 4.97 | 1.36 |
| 22:00 | 1491 | Sao Paulo vs Cuiaba MT | 1.45 | 3.76 | 6.83 |
| 22:00 | 3766 | Tenerife vs Malaga | 1.67 | 3.41 | 5.33 |
| 22:15 | 3847 | Stjarnan vs Valur | 3.15 | 3.68 | 1.96 |
| 22:30 | 3656 | Vitoria Guimaraes vs Gil Vicente | 2.16 | 3.47 | 3.08 |
| 23:30 | 4882 | Coritiba vs America Mineiro MG | 2.09 | 3.26 | 3.17 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 15, 2022

Nipashe



Lukaku: Siondoki Chelsea

UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga wakijinoa kuelekea mchezo dhidi ya Dodoma Jiji. **PICHA: YANGA**

## ...Mayele atuliza presha mashabiki

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele ameshusha presha za mashabiki wa klabu hiyo amesema yuko kwa ajili ya timu hiyo na atahakikisha anakata kiu yao katika michezo iliyobakia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mayele katika michezo mitatu hajafunga na wala timu yake ya Yanga haijapata ushindi katika mechi hizo na leo wanacheza dhidi ya Dodoma jiji FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayele alisema yaliyotokea katika michezo mitatu iliyopita ni mapito na wanajiandaa kwa ajili ya mchezo ujao anawafurahisha mashabiki wao.

Alisema yuko kwa ajili ya kusaidia timu yake kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao kwa kufikia malengo ya kutwaa taji la ubingwa.

"Nipo kwa ajili ya Yanga na wanayanga watulie watafurahi, bado tuna michezo mingine iliyopo mbele yetu, tunapambana kutafuta ushindi ili kujihakikishia malengo yetu ya kutwaa ubingwa wa ligi msimu huu," alisema mshambuliaji huyo.

Alisema ana matarajio makubwa mechi zijazo wakianza na Dodoma jiji FC kupata ushindi kwa sababu Kocha ( Nesreddine Nabi) amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo mitatu iliyopita ambayo hawakupata matokeo ya ushindi.

# Yanga, Dodoma hapatoshi leo

## Yanga inatafuta pointi tatu muhimu ili ijiimarishe kileleni kwenye mbio za ubingwa, huku...

**Na Adam Fungamwanngo**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kucheza mechi ya raundi ya 24 dhidi ya Dodoma Jiji, pambano litakalofanyika saa 10:00 jioni, badala ya saa 1:00 usiku kama ilivyopangwa awali.

**Yanga itakuwa na kazi mbili kwenye mechi ya leo, kusaka pointi tatu ambazo zinaisogeza karibu na ubingwa, huku pia ikitaka kupoza wanachama na mashabiki wake ambao wameonekana kuwa na mhaho, baada ya suluhu tatu mfululizo.**

Juzi jioni, Bodi ya Ligi ilitoa taarifa kuwa mechi hiyo namba 208, sasa itachezwa saa 10:00 jioni badala ya saa 1:00 usiku kama ilivyopangwa awali kutokana na uwanja huo kuwa na matumizi kesho, ambapo maandalizi ya shughuli hiyo yanatakiwa kufanyika kuanzia leo usiku, hivyo kusababisha mechi hiyo kurudishwa nyuma ya muda.

Itakuwa ni mechi ya kisasi kwa Dodoma Jiji kwani Desemba 31 mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilikubali kupigo cha mabao 4-0.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amesema kuwa kikosi kiko tayari, lakini kukiwa na wasiwasi wa kipa Djigui Diarra na Abobakar Salum 'Sure Boy' kutokuwemo kwenye kikosi hicho, huku Djuma Shaaban na Khalid Aucho wakiwa wamepona majeraha yao.

"Maandalizi yapo vizuri, tunakwenda kucheza mechi hii kwa tahadhari kutokana na matokeo yetu ya mechi za mwisho, hayakuwa mazuri, lakini tumejiandaa kuhakikisha tunarudi kwenye wakati wetu mzuri. Tuna nafasi nzuri bado ya kufikia malengo yetu, ila kuna kitu cha ziada kinatakiwa kufanyika, mechi iliyopita hatukuwa na bahati, tulikosa mabao mengi na penalti pia," alisema Kaze.

Akizungumzia hali ya wachezaji wake, alisema baadhi ya majeruhi wanaendelea vizuri, lakini akiwa hana uhakika na wengine kama watakuwemo.

"Djuma Shaaban na Khalid Aucho wamepona majeraha yao, wapo vizuri na huenda wakawemo kwenye kikosi, lakini sina uhakika kwa Djigui Diarra, ingawa anaendelea vizuri, na Aboubakar Salum ambaye yeye alikuwa anaumwa malaria, tutaangalia itakavyokuwa, lakini waliobaki wapo vizuri na wanajua jukumu lao la kurudisha hali ya kujiamini wao wenyewe na kwa mashabiki," alisema kocha huyo msaidizi.

Mchezaji Deus Kaseke amesema wao kama wachezaji matokeo yaliyopita wameyasahau na wanachoangalia ni mechi inayofuata.

"Ukicheza na timu kubwa kama Yanga kila mechi yanahitajika matokeo ya ushindi, na nilazima mchezaji uweze kuhimili presha ya mashabiki, wanachama na hata viongozi. Hiko ni kipindi ambacho kila timu duniani huwa inapitia, siyo Yanga tu, lakini mara nyingi huwa ni kwa kipindi kifupi. Naamini leo itakuwa ndiyo mwisho wa timu kutoa sare," alisema Kaseke.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji Mohamed Omar Muya amesema kuwa wamejiandaa kikamilifu na mechi hiyo.

"Tunafahamu mechi ya kesho ni mechi ngumu, wao wanaihitaji, lakini na sisi tunaitaka pia, hatujapishana sana na wenzetu, tunaweza kumaliza tukiwa kwenye nafasi ya nne kama tunafanya vizuri. Tunayo nafasi ya kufikia malengo tuliyonayo wakati ligi inaanza. Tunaiheshimu Yanga, ubora wao, kikosi chao, uwekezaji wao, lakini na sisi pia tuna wachezaji vijana ambao wanahitaji kufika mbali ambao wanaelewa dhamana wanaoibeba kwenye timu ili waweze kujitambua na kupambana kwenye mechi hii kubwa," alisema kocha huyo.

Yanga ilitoka suluhu mechi tatu mfululizo dhidi ya Simba, Ruvu Shooting na Prisons, lakini ikiwa kileleni kwa pointi 57, wakati Dodoma Jiji iko kwenye nafasi ya nane kwa pointi 28.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >